# Nipashe

Ijumaa Machi 8, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581609

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


**BOT** yaanika kasi ya kutisha wizi wa mabilioni njia ya mtandao

UKURASA 3



**NHIF**, hospitali binafsi kukutana ili kuwekana sawa

UKURASA 4

**MBOWE** akimbilia mahakamani kuzuia nyumba kupigwa mnada

UKURASA 7



**JORGINHO** alifurahishwa kuhusishwa Barcelona

UKURASA 22

## SIKU YA WANAWAKE

# Sauti zasikika toka kila kona

**WATAKA** nguvu zaidi fursa, uongozi; daktari, nahodha, dereva bodaboda waeleza tamu chungu za kazi zao... *Endelea ukurasa wa 2, 5, 12*



**"Kwa hiyo nikimwangalia huyu nilimfanyia upasuaji akiwa mtoto mchanga kabisa, sasa leo na yeye ameniletea mtoto wake, inaniambia ni kweli nimekuwa katika kazi muda mrefu. Inanipa hamasa, wengine nakutana nao hata siwakumbuki,"Dk. Ngiloi.**

**"Ninawaasa wanawake wakuu wa taasisi, mashirika na vyuo vya umma nchini, kuanzisha na kuunga jitihada za program za kuinua wanawake katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kwenye ngazi za mamlaka mnazozisimamia,"alisema Dk. Gwajima.**

**"Wanawake tusitambie vyeo vyetu bali tuwasaidie wengine na kutohofia kutekeleza majukumu ya aina yoyote yaliyo mbele yetu kwasababu ya kuhofia jinsia zetu,"alisema Dk. Makakala.**

**"Mtu anapokwambia wekeza kwa mwanamke ni kuendeleza maendeleo ya jamii na ustawi wake. Maana yake tayari kumeonekana kuna upungufu wa uwekezaji,"Rutazaa**

**"Pia muwe wasikilizaji, tunajifunza kwa Rais Samia amekuwa akisiliza na kutoa nafasi ya mtu kufanya, hana papara katika sehemu anayotakiwa kuwa na presha ya maamuzi, huu ni mfano mzuri kwa wanawake viongozi, jishusheni kwa wale mnaowaongoza, wasaidieni shida zao ili nao wanyanyuke," alisisitiza Balozi Amina.**

**"Dunia ya sasa hivi imebadilika tunataka kuwa na jeshi la wanawake likiwa kidijitali...hii itasaidia kujua tuna wanawake wangapi na jinsi ya kuweza kuwasaidia,"Jokate.**



Nahoza wa boti mwanamke, Bahati Issa Suleiman (mwenye kilemba cha njano), akiwasafirisha watalii kuelekea kwenye visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**Mwendesha bodaboda aliyeanza vita maisha akiwa 'hausigeli' Dar**

UKURASA 14

**MICHEZO** **KOCHA SIMBA ALIA UZEMBE** UK. 24

**KATUNI** UK. 6

SIKU YA WANAWAKE

# Sauti zasikika toka kila kona

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani leo, maoni tofauti yametolewa nchini yakiwamo ya kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuendelea kuongeza idadi yao kwenye uongozi, huku wengine wakilia ukatili, mirathi na umiliki mali kuwa bado tatizo kubwa.

Wakizungumza na waandishi wetu katika maeneo mbalimbali nchini, wanawake hao walisema ni miaka 29 tangu kuanza maadhimisho hayo, hatua kubwa zimepigwa, lakini bado kuna changamoto zinazopaswa kupewa kipaumbele ili kuondoa kikwazo kwenye ustawi wa wanawake.

**MOROGORO**

Mkazi wa Kata ya Kichangani, Anna Kisimbo ameiomba serikali kusimamia wanawake katika upatikanaji wa haki hasa kwenye masuala ya mirathi kwa kuwawekea watetezi wa kujitolea wanaoweza kuwasaidia kusimamia haki zao jambo ambalo limekuwa mwiba licha ya kuwapo kwa usawa wa kijinsia na idadi kwa sasa.

Mjasiriamali Adrian Banzi, aliishukuru serikali kwa kuboresha masuala ya usawa wa kijinsia kwa sasa unaosaidia hata kimapato baina ya mwanamke na mwanamume na hivyo kukuza uchumi wa familia, tofauti na iliyokuwa katika miaka 1950 hadi 1980 wakati baba alikuwa mfanyakazi pekee na familia kuendelea kuwa maskini akizidiwa na majukumu.

Wameomba Rais Samia aongeze kasi kutoa kipaumbele cha uongozi katika nafasi za uongozi hasa kwa wanawake vijana.

Milika Mhamaka, mkazi wa Kihonda Morogoro, alisema licha ya kutoa nafasi ikiwamo za wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa, wakurugenzi na wakuu wa taasisi mbalimbali ikiwamo Uhamiaji, lakini aongeze kasi hiyo.

"Binafsi nampongeza sana Rais Samia kwa kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake hasa vijana hata pale unapoona kuna kiongozi mkubwa mwanamume utaona anayefuatia ni mwanamke tena ni kijana tunaomba aongeze kasi zaidi," alisema Milika.

**KASKAZINI**

Wanawake wa Arusha na Kilimanjaro, wamesema tangu kuanzishwa kwa siku ya wanawake duniani, Tanzania imepiga hatua moja kubwa pekee katika masuala ya uongozi, lakini bado wameachwa nyuma katika mchakato mzima wa maamuzi na umiliki wa mali.

Aginatha Rutazaa, Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la TUSONGE, Moshi, mkoani Kilimanjaro, alisema upungufu wa uwekezaji kwa mwanamke, ambao unalenga kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii, jambo hilo bado linapaswa kuboreshwa zaidi, ili kuwa na ushiriki wa pamoja katika mchakato wa maendeleo.

"Mtu anapokwambia wekeza kwa mwanamke ni kuendeleza maendeleo ya jamii na ustawi wake. Maana yake tayari umeonekana kuna upungufu wa uwekezaji.

"Na upungufu huo ndio haya tunayosema yanatokana na mifumo, taratibu, mitizamo iliyojengeka ndani ya jamii na imani, zimeona kwamba huyu, labda hawezi kufanya hiki na haruhusiwi kufanya hiki.



Mchuuzi wa vitunguu, maarufu kwa jina la Mama Anna, akiviandaa wakati akisubiri wateja katika Soko la Samunge, jijini Arusha jana. Bei ya vitunguu imepanda kutoka 10,000/- hadi 18,000/- kwa kipimo cha ndoo ndogo ya ujazo wa lita tano. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

Apaisaria Meena, mkazi wa Himo, Wilaya ya Moshi, alisema kupitia siku ya wanawake, wanataka serikali ije na mpango mahususi wa kuhakikisha wanawake wanachaguliwa katika nafasi za maamuzi na sio kuteuliwa.

Faustina Urio, Mkazi wa Manispaa ya Moshi, alisema," Sisi hatujui kuhusu siku ya wanawake, ila kama ipo itumike kuwafundisha wanawake vijana juu ya kuwa wavumilivu kwenye ndoa, na kuwasaidia waume zao katika kuleta maendeleo.

Mkazi wa Rombo, Elizabeth Mroso, alisema kwa sasa bado siku hiyo haina matokeo chanya, huku akiitaka serikali kuboresha sera na sheria zitakazomlinda mwanamke katika uzalishaji mali.

Wakati, Hadija Hamisi, mkazi wa Morombo jijini Arusha, anasema wanawake wa vijijini wengi wao hawajui kuhusu maadhimisho hayo, kwa kuwa wanaona yamewalenga zaidi wanawake wa mjini na wenye kipato, kwa sababu ndio hushirikishwa juu ya hilo.

Mkazi wa Olasiti, Zulfa Mfinanga, alisema maadhimisho hayo yamesaidia kupanda kwa nafasi ya mwanamke katika uongozi, kujikomboa wanawake kiuchumi, kupatikana nafasi za wanawake kwenye harakati za maendeleo pamoja na kuimarisha mifumo ya sekta za elimu na afya.

Wakili Mary Mwita, anasema maadhimisho hayo yamefungua wanawake wengi akili, na kuwa na uwezo wa kupaza sauti kudai haki zao, kama vile haki ya kumiliki ardhi, uhuru wa kutoa maoni, kupinga ukatili dhidi ya mwanamke na mtoto wa kike.

**KATIBU UWT TAIFA**

Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jokate Mwegelo, amezindua kampeni maalumu ya kuhamasisha wanawake na wasichana kujisajili na umoja huo kidijitali, huku akitaka wengi kuendelea kumuunga mkono Rais Samia kutokana na jitihada za maendeleo anazozifanya.

"Dunia ya sasa hivi imebadilika tunataka kuna jeshi la wanawake likiwa kidijitali...hii itasaidia kujua tuna wanawake wangapi na jinsi ya kuweza kuwasaidia.

"Tumetoa maagizo kwa makatibu wa kila mikoa kulisimamia hili kuhakikisha wanawake wote wanajisajili. Na tunatoa wito kwa wanawake nchi nzima kujitokeza kwa wingi kujisajili kidijitali," alisema Jokate.

**DODOMA**

Wananchi mkoani Dodoma wamesema kuwa tangu kuanza kwa maadhimisho ya siku ya wanawake duniani kumekuwapo na mabadiliko makubwa, ikiwamo kuongezeka kwa uelewa nafasi ya mwanamke katika jamii na kushirikishwa kwenye ngazi mbalimbali za maamuzi.

Christopher Dioniz, alisema uwapo wa maadhimisho hayo umewezesha nchi kupiga hatua kwenye usawa wa kijinsia kutokana na ongezeko la wanawake katika ngazi za maamuzi nchini huku akishauri

serikali kuweka utaratibu wa kufanya shunguli mbalimbali zinazohusu siku hiyo maeneo ya vijijini.

Mkazi wa Kijiji cha Chikuyu Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, Evarin Yohana alisema bado kuna tatizo la kukosa elimu kwa wanawake waishio vijijini ndiyo maana wanashindwa kushiriki kikamilifu katika siku hiyo na kudai kuwa bado kuna mfumo dume unaowakandamiza wanawake.

Mkazi wa Kijiji cha Kigwe Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Frola Kisanga, alisema siku ya wanawake duniani ipo kwa manufaa ya baadhi ya wanawake hasa wa mijini na sio vijijini huku wa vijijini wakikosa fursa ya kuitumia siku hiyo kueleza kero zinazowakabili kama vile ukosefu wa maji salama kutembea umbali mrefu kufuata huduma za kiafya na mfumo dume unaowakosesha haki ya kumiliki mali.

**WAZIRI GWAJIMA**

Aidha, Dk. Doroth Gwajima, amewaasa wanawake wakuu wa taaasisi, mashirika na vyuo vya umma nchini, kuanzisha na kuunga jitihada za programu za kuinua wanawake katika shughuli mbalimbali za kiuchumi katika ngazi za mamlaka wanazosimamia.

Akifungua mkutano wa mkutano wa wanawake wakuu wa taasisi, mashirika na vyuo vya umma waliokutana kwa lengo la kujadili mambo mbalimbali yanayowahusu wanawake katika ngazi za maamuzi ikiwa ni katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, aliwataka wanawake kumuunga mkono Rais Samia aliyewekeza wao.

Alisema kaulimbinu ya mwaka huu, inayosema, 'Wekeza kwa Mwanamke: Kurahisisha Maendeleo kwa Mwanamke na Taifa kwa ujumla', inalenga wanawake hao walio katika ngazi za maamuzi kuwashika mkono wanawake wanaochipukia na kuwasaidia kufikia ndoto zao.

Mgeni Maalum katika tukio hilo, Balozi Amina Salim Ali, aliwataka wanawake wenye nafasi za juu kuwasaidia kwa mawazo, hali na mali wanawake wanaowaongoza badala ya kutumia mamlaka zao kuwadidimiza.

Kamishna Jenerali wa Idara ya Uhamiaji, Anna Makakala, aliwataka wanawake kutotambia vyeo badala yake wasaidie wengine na kutohofia kutekeleza majukumu ya aina yoyote yaliyo mbele yao kwa sababu ya kuhofia jinsia zao.

Mkazi wa Ukonga Majumbasita, Juma Mang'ang'a, alisema wanawake wameendelea kutambua nafasi yao katika jamii, kuna tofauti katika kila mwaka, huku akitaka maadhimisho hayo kuzingatia wanawake wa pembezoni.

**SONGEA**

Wilayani Namtumbo wanawake wamesema bado kuna matukio ya ukatili wa kijinsia hasa maeneo ya vijijini jambo ambalo linapaswa kupingwa vikali.

Walisema katika maeneo mengi wanawake wananyimwa uhuru wa kutoa maamuzi kuhusu kupanga mapato na matumizi ya mazao wanayozalisha, kufanya kazi bila kupumzika, kutelekezwa na kunyang'anywa mali.

Afisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Peres Kamugisha pamoja na kuwapongeza wanawake wa Wilaya ya Namtumbo kwa kuadhimisha siku ya wanawake kiwilaya, aliitaka jamii kuwekeza katika watoto wa kike akiamini kuwekeza kwa mtoto wa kike kuna faida kubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Ngollo Malenya aliwataka wanawake wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uchaguzi mkuu kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuwa ni haki yao kikatiba.


NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street
P. O. Box 6100
Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045
Fax: +255 22 2112045
info@transmark-tz.com
www.transmark-tz.com

DEV RECOVERIES LIMITED

TANGAZO LA UUZAJI WA MALI KWA NJIA YA ZABUNI

Kampuni ya **DEV RECOVERIES LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED** kupitia barua ya miadi ya tarehe 02/03/2024, tunapenda kuutangazia umma juu wa uuzaji wa mali zilitotajwa hapo chini kwa njia ya **ZABUNI.** Wazabuni wanaohitaji, wanaalikwa kuleta zabuni ndani ya siku 14 kwa ajili ya ununuzi wa mali katika bahasha iliyofungwa na iliyoandikwa juu **"ZABUNI KWA AJILI YA UNUNUZI WA MALI HUSIKA"** inaonyesha ofa ya mali hiyo yenye anuani kamili ya mzabuni na pia iwasilishwe katika anuani iliyoko chini kabla ya saa 10:00 jioni, tarehe 21/03/2024 katika ofisi zilizotajwa hapo chini. Wazabuni wanaalikwa kuhudhuria siku ya tukio kama watapenda.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA .**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | MAELEZO | TAREHE YA KUFUNGULIWA ZABUNI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SHULE YA SEKONDARI ARUSHA CITY | Namba ya kiwanja. 167, Eneo la Olasiti. CT na.37000 LO na. 312992 | Shule ya Sekondari. Eneo la mraba 9,247. Jengo lina Madarasa, Ofisi, Mabweni na Maabara. | 21/03/2024. Saa 10:00 Jioni |
| 2. | TEMI INVESTMENT LIMITED | Kiwanja na.67,Kijiji cha Olosiva, Arusha. CT na.24132, Lo na. 308060 | Eneo la biashara lenye, Pampu ya mafuta, Kisima cha majisafil,Maghala na n.k. | 21/03/2024. Saa 10:00 Jioni |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
2. Wazabuni wanatakiwa wakumbuke kwamba, taarifa zilizotolewa humu ni bila ya dhima ya muuzaji katika usahihi wa tathmini na ukaguzi wa mali unashauriwa.
3. Muuzaji hatolazimishwa kukubali zabuni ya juu kabisa au yeyote.
4. Mzabuni atakayefanikiwa kushinda, atalazimika kulipa 25% ya bei ndani ya siku 4 ya tarehe ya ushindi wa zabuni na baki ilipwe ndani ya siku 14 au kama mzabuni aliyeshinda amekubaliana na benki kwa ajili ya taratibu za malipo. Kama itatokea baki haikulipwa ndani ya siku 14 au benki aliyokubaliana nayo mzabuni haijalipa baki hiyo, muuzaji atabatilishwamalipo ya 25% yaliyolipwa awali na mzabuni mwingine atapewa nafasi ya kununua mali.
5. Wazabuni ambao wana shauku ya kuiona na kuikagua mali wanaruhusiwa kufanya hivyo, kulingana na uteuzi na idhini ya awali ya dalali wa Muuzaji katika anuani za chini.
6. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
7. Zabuni inatakiwa itumwe kwenye anuani ifuatayo

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**KAMPUNI YA DEV RECOVERIES LIMITED**
**NIC LIFE HOUSE, GHOROFA YA 4**
**SOKOINE DRIVE/ MTAA WA OHIO,**
**P.O.BOX 6707, DAR ES SALAAM**
**Mobile; 0788438640/0712073680**
**Whatsapp only +255712390460/ +255782065914**

HABARI KITAIFA

# BoT yaanika kasi ya kutisha wizi wa mabilioni mtandaoni

Na Christina Mwakangale



Gavana wa Benki Kuu, Emmanuel Tutuba.

WATUMIAJI wa huduma za kifedha mtandaoni na katika taasisi za kifedha, wametoa maoni tofauti kuhusu wizi wa fedha kutoka kwa watoa huduma hizo huku zaidi ya Sh. trilioni moja ndani ya mwaka mmoja zikibainika kuibwa na wajanja hao.

Miongoni mwa waliotoa maoni hayo ni walioko katika mfumo usio na ulio rasmi ambao wamesema huhifadhi fedha zao kwenye mifumo rasmi ya kifedha kama vile mitandao ya simu na benki.

Machi 5, mwaka huu, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ilitoa taarifa yake kwenda kwa benki, taasisi za fedha na wenye mifumo ya malipo kuhusu kuwapo kwa ulaghai huo huku kwa kipindi cha misimu iliyoigawanya kwa vipindi vinne, kuanzia Machi, Juni, Septemba na Desemba, 2023.

taarifa ya BoT inaonyesha vitendo vya 'ukwapuaji' fedha mtandaoni viliongezeka kwa asilimia 60 kupitia mashine za kutolea fedha (ATM) huku ujambazi wa kutumia silaha ukiwa na takwimu sifuri.

Mariam Mwakaje, mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, akizungumza na gazeti hili jana, alisema ametumia huduma za kifedha kwa miaka kadhaa na ilipoingia mfumo wa kuhifadhi fedha kwa njia ya mtandao, amekuwa akitumia huduma hiyo zaidi kuliko benki.

"Ninafanya shughuli nyingi za miamala kulingana na shughuli zangu kupitia benki mitandao. Yaani kila kunapokucha naweka Sh. Milioni tatu katika kila kampuni ili akitokea mteja ana mzigo na anahitaji nimlipe kwa kampuni fulani ya simu, namtumia.

"Na kwa ubize nilo nao hasa kuanzia asubuhi hadi saa 2:00 usiku, sina muda wa kuangalia salio. Kama kuna kiwango kinachotwa, pengine nami nimeshatendewa sana hilo, BoT ndio wametuthibitishia, kwa taarifa hii," alisema Mwakaje.

Brighton, aliyejitambulisha kwa jina moja, mkazi wa Ilala, mtumishi wa umma, alisema malipo ya mshahara hupokea kupitia benki na hana muda wa kuangalia salio, hivyo kuna uwezekano wa pesa ndogo kuondolewa kwenye akaunti yake bila yeye kujua.

"Mfano mtu anachukua Sh. 200 katika akaunti yangu si rahisi kujua kwa sababu akauti yangu inakuwa na tarakimu kuanzia sita na kuendelea, ikitolewa pesa hiyo ndogo utajuaje? Jiulize watu wenye akaunti benki fulani labda 100 kila siku wakichukuliwa katika akaunti zao Sh. 200 kila mmoja utajuaje?," alihoji.

Mjasiriamali wa samaki, Amina Bwalya, mkazi wa Gongo la Mboto, alisema anaamini fedha zake ziko salama katika mitandao ya simu kwa kuwa kila siku baada ya biashara yake, huweka katika simu Sh. 6,000.

"Mimi kama kufanyiwa vitendo vya wizi katika fedha zangu mtandaoni, nitakuwa nimefanyiwa sana na sijui kwa sababu fedha ninayoweka kila siku hasa siku tano za wiki,

"Nakuja kuitoa hiyo fedha, ninapokuwa na shida, sina kumbukumbu wala kitabu cha kunukuu jumla ya fedha ninazoweka katika simu, hata meseji huwa nafuta ukipita muda fulani," aliongeza.

Mmoja wa wafanyakzi katika kampuni binafsi, Marcus Philemon, alisema: "Ninachojiuliza kwamba kama wafanyakazi wa ndani wa taasisi, benki, mitandao ya simu, wanauwezo wa kukwapua mamilioni ya fedha sisi ni nani, BoT itulindie fedha zetu.

**TAARIFA YA BoT**

Machi 5, mwaka huu, BoT ilisema robo ya kwanza ya mwaka hadi Machi, 2023, Sh. 2,427,166,459 ziliibwa kupitia wafanyakazi wa ndani wa taasisi za fedha, benki mtandao, ATM na hundi zilizoghushiwa.

Pia ilibaninika kwamba ulaghai wa fedha hizo za wateja, kupitia mitandao ya simu inayofanyika Sh. Milioni 674.062 ziliibwa kwa kipindi cha Juni, 2023 huku matukio hayo yakiongezeka kwa asilimia 84, Desemba mwaka huo na kufikia Sh. bilioni 1.654.

Aidha, Septemba, 2023 matukio ya fedha zilizokwapuliwa yakihusisha wafanyakazi wa ndani yalisababisha wizi wa Sh. bilioni 1.350.

BoT ilisema kwa kipindi chote cha robo nne katika mwaka 2023, vitendo vya fedha 'kukwapuliwa' kwa ujambazi wa kutumia silaha havikutokea kwa mwaka huo.

Aidha, kwa robo ya Juni 2023, ilionyesha Sh. 2, 555,036,2066 zilikwapuliwa kwa muundo tofauti, huku Septemba mwaka huo, Sh. 2,674,670,828 na Desemba Sh. 2,641,148,362 zikibwa pia.





Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay (kulia), akipokea tuzo ya Super Brands kwa niaba ya benki hiyo, kutoka kwa Mkurugenzi wa Super Brands Afrika Mashariki, Jawad Jaffer (katikati) na Meneja Biashara wa Nation Media Group, James Sogoti (kushoto), katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NHIF, hospitali binafsi kukaa meza moja

**Na Maulid Mmbaga**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unatarajia Jumatatu ijayo kukutana na wamiliki wa hospitali binafsi kutafuta suluhu ya hoja zao juu ya kitita kipya ambacho walikilalamikia hadi kutishia kusitisha huduma za matibabu.

Wiki iliyopita takribani hospitali binafsi saba, zilitangaza kusitisha huduma kwa wanachama wa NHIF kwa madai ya kutokukubaliana na kitita kipya kilichoanza kutumika Machi Mosi, mwaka huu.

Wamiliki hao walisema katika kitita kipya kilichopendekezwa na mfuko huo bei zimeshuka kwa kati ya asilimia 20 na 30 wakati thamani ya dola, dawa na ya uwekezaji zikiwa zimepanda.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Benard Konga, alisema baada ya hospitali hizo kutangaza kugoma, mfuko ulichukua hatua ya kuangalia wanachama walioko kwenye vituo husika na kuhakikisha wanaendelea kupata huduma.

Hatua ya pili waliyochukua ni kuwaelekeza wanachama waliofika kwenye vituo hivyo kwenda vituo vingine na hatua ya tatu ni kuwatafuta wangonjwa wenye magonjwa makubwa kama ya figo na kuwaeleza hali halisi iliyoko na kuwashauri nini cha kufanya ili waendelee kupata huduma.

"Kila asubuhi sisi tulikuwepo kwenye hayo maeneo ili akitokea mtu mwingine tunamhamisha na kumpeleka sehemu nyingine kwa sababu lazima tuwatumikie wanachama. Baada ya hapo, walikaa na Waziri (wa Afya) Ummy Mwalimu na kuwasihi waendelee kutoa huduma, wakati jitihada za majadiliano zikiendelea.

"Ninaamini tutakapokaa tutapata mwafaka na kwa yale maeneo ambayo kweli yana changamoto yatarekebishwa na yanayohitaji ufafanuzi utatolewa," alisema.

Pia alisisitiza kuwa sekta binafsi wanaitambua, wanaithamini na kushirikiana nayo na hawataacha kufanya hivyo kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma wanazozitoa kwa maslahi ya wananchi wanufaika wa mfuko na taifa kwa ujumla.

Kuhusu jitihada kukomesha udanganyifu, Konga alibainisha kwamba wamefanya utafiti 596 na kuokoa takribani Sh. milioni 200. Pia alisema walisitisha mikataba 42, kubaini wanataaluma 178 waliofanya udanganyifu ambao tayari wamewaripoti kwenye mamlaka zao.

"Pia tumefungua mashtaka yanayohusu wanachama 68 juu ya matumizi mabaya ya kadi, na jumla ya kadi 5,468 zimesitishiwa huduma kutokana na kuwa na viashiria vya kuhusika katika udanganyifu.

Pia kuna taarifa inasambaa kwamba watumishi 147 wamejihusisha na udanganyifu, lakini kati yao 27 ndio wa mfuko.

"Wamechukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma, 16 wamefukuzwa kazi, watano wamepewa onyo, wawili wameshushwa mshahara na wanne wameshushwa vyeo, lakini pia kuna waajiri binafsi pia ambao wamesitishiwa mikataba yao," alisema Konga.

**CHANGAMOTO**

Alibainisha kuwa ubora wa huduma zinazotolewa kwenye vituo vya afya hasa vijijini, ni moja ya changamoto inayowakabili. Alisema mtu akienda na kadi ya bima kwenye vituo anaona ni bora aiweke mfukoni atoe fedha zake ili apate huduma na kwamba kutokana na huduma zilizoboreshwa kwa sasa malalamiko yamepungua.

Nyingine ni kuongezeka kwa gharama za matibabu na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yanatumia fedha nyingi kuyatibia, akieleza kwamba yanarudisha nyuma nguvu kazi katika ngazi binafsi kama familia na taifa, huku akisisitiza watanzania kujitahidi kuyaepuka.

"Uelewa juu ya umuhimu wa bima ya afya bado ni kikwazo, hivyo elimu bado inahitajika kutolewa kwa kuwa wananchi wengi hawaoni haja ya kukata bima zaidi ya kusubiri augue.

"Kinachofanyika sasa ni kuboresha muundo wa shirika ili kukidhi matakwa ya sheria ya bima ya afya kwa wote, kuongeza wigo na mtandao wa vituo vya kutolea huduma ya afya, kuendelea kushirikiana na wadau wa maeneo yote ili kuimarisha ushirikiano na kuhakikisha mfuko unakuwa kinara kwa jamii," alisema Konga.

# Biteko: Mgawo umeme umefika mwisho

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ametangaza kwamba mgawo wa umeme ambao umedumu kwa muda mrefu uko mwishoni kumalizika.

Amesema tangu Februari 22, mwaka huu, hakuna mgawo wa umeme kama ilivyokuwa kabla na akisisitiza kwamba kauli yake hiyo si ya maneno bali itadhibitika kwa vitendo.

Akizungumza wakati wa hafla ya kugawa vifaa na majiko ya nishati safi ya kupikia kwa wanawake wa Mbagala, Biteko alisema mipango ambayo serikali imeiweka kumaliza tatizo hilo imefikia tamati.

"Changamoto ya umeme iko mwishoni si kwa sababu ya kutamka tu na tungependa tusiseme sana, bali matendo ndiyo yaseme zaidi.

"Ninyi ni mashahidi. Tumekuwa kwenye mgawo kwa muda mrefu na ndio maana tangu tarehe 22 mwezi uliopita, hakuna mgawo wa umeme. Maana yake ni kwamba mipango ambayo serikali imeweka ya kuhakikisha tunapata umeme wa uhakika imefika mwishoni na imetuletea matokeo," alisema.

Dk. Biteko alisema wanafahamu kuna changamoto kubwa ya miundombinu ya kusafirisha umeme na kwamba tayari wameshaanza kubadili mfumo kutengeneza miundombinu ya kupitisha umeme chini ya ardhi.

"Kuna baadhi ya maeneo tunabadilisha miundombinu kwa kujenga 'cable' ya kupitisha umeme chini kwa chini mfano Kurasini ambao utakwenda wilaya ya Ilala na lengo ni kuhakikisha tunapata umeme wa uhakika, tulivu na usio katikakatika," alisema Dk. Biteko.

Alisema mbali na miundombinu, kuna sababu mbalimbali zinazochangia upungufu wa umeme ikiwamo ongezeko la watu na uharibifu wa vyanzo vya maji unaotokana shughuli za binadamu ikiwamo matumizi ya kuni na mkaa ambao unatokana na ukataji miti.

Naibu Waziri Mkuu aliagiza mamlaka zinazohusika na usimamizi wa vyanzo vya maji ikiwamo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania((TFS) kudhibiti ukataji wa misitu.

Aliwaomba wadau mbalimbali zikiwamo kampuni zinazozalisha vifaa vya nishati safi kujitokeza kushirikiana na serikali kufanikisha mpango mkakati wa matumizi ya nishati safi.

Biteko aliipongeza Kampuni ya ORXY kwa kuungana na serikali katika kampeni hiyo kugawa vifaa na majiko ya nishati safi ya kupikia kwa makundi mbalimbali ya akina mama.

"ORX wametoa mfamo mzuri sana, katika kuunga mkono jitihada hizi za serikali za matumizi ya nishati safi. Wamekuwa wakigawa majiko ya gesi kwa makundi ya kinamama hasa hawa wanaojihusisha na biashara ya mama ntilie na leo (jana) wamegawa tena 100. tunapongeza sana kwa hili," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa ORYX, Benoit Araman, alisema wako tayari kushirikiana na serikali kufanikisha kampeni hiyo kwa kupitia kugawa vifaa vyao kwa makundi mbalimbali ambayo yako tayari kubadilika na kutachana na nishati chafu na kutumia nishati safi.

"Tunafahamu kwamba matumizi ya nishati safi yanachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu afya za watu hasa kundi la wanawake ambao ndio watumiaji wakubwa, kwa hiyo sisi tuko tayari kushiriki kusaidia katikankuokoa afya zao.

# Mpango aagiza kuimarishwa sekta fedha kuhimili misukosuko uchumi

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MAKAMU wa Rais, Dk Philip Mpango, amewaagiza viongozi na wataalamu katika sekta ya fedha nchini, kuhakikisha uwezo wa taasisi na sekta nzima unaimarika ili kuhimili misukosuko inapotokea.

Pia ameagiza kuangalia namna bora ya kuimarisha idara na vitengo vya utafiti na masoko ya kifedha ili kuimarisha uhimilivu wa sekta za kifedha.

Dk. Mpango alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua kongamano la 21 la Taasisi za Fedha kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan lenye kaulimbiu "Kuimarisha Ustahimilivu wa sekta ya fedha nyakati za changamoto za kiuchumi."

Alisema kongamano hilo litajadili na kupendekeza namna ya kuimarisha maeneo ya menejimenti ya vihatarishi, usimamizi makini na ufuatiliaji wa mienendo ya benki moja moja na sekta nzima ya fedha kwa kuwa ni muhimu katika kujenga sekta imara na yenye uwezo wa kuhimili misukosuko.

"Kutokana na umuhimu huo naiagiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na taasisi zote za fedha kutobweteka kwa sababu dhoruba za kiuchumi duniani bado zinavuma kwa nguvu na kuna maeneo duniani bado yana changamoto. Hatuna budi kupitia mara kwa mara sheria, kanuni na mwongozo wa taasisi za fedha ili kubaini maeneo yenye udhaifu na kufanya maboresho stahiki.

"Pia nawaomba washiriki wa kongamano hili kutafakari kwa kina changamoto ya uhaba wa fedha za kigeni uliopo hivi sasa na hatua gani za muda mfupi na wakati, ambazo zinabidi zichukuliwe zaidi ya hatua za urekebu zinazochukuliwa na BOT," alisema.

Alisema ni vyema washiriki wakajadili nafasi ya kutumia viwango nyumbufu vya ubadilishaji fedha katika kudhibiti uhaba wa fedha za kigeni nchini.

"Upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu ni muhimu katika ukuaji wa uchumi lakini gharama za mikopo katika soko la Tanzania bado ni kubwa.

" Licha ya uwiano wa mikopo chechefu kwa mikopo yote kupungua bado uwiano huo uko juu ya ukomo wa asilimia tano ambao umewekwa na BoT, hivyo kongamano hili linapaswa kuangazia njia ya kudhibiti mikopo chechefu, kupunguza gharama za mikopo na kupanua wigo wa mikopo nafuu, hasa wajasiriamali wadogo, wakubwa na wa kati katika sekta za kilimo mifugo, uvuvi, uchimbaji wa madini na viwanda vidogo," alisema.

Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, alisema uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi na pato la taifa bado uko chini kulinganisha na wastani wa kikanda.

Alisema katika mwaka 2021/22, wastani wa Tanzania ulikua asilimia 18.2 kulinganisha na asilimia 25.3 katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na asilimia 26.6 kusini mwa jangwa la Sahara

Pamoja na hayo, alipongeza mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha hivi karibuni, yalioongeza idadi ya watu wanaotumia huduma rasmi za fedha nchini hadi kufikia asilimia 76 mwaka 2023 kutoka asilimia 65 mwaka 2017.

"Hii ni hatua kubwa ambayo sote tunapaswa kujivunia. Aidha, mikopo iliyotolewa na benki kwa sekta binafsi imeongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha baada ya UVIKO-19. Kwa mfano kwa mwaka 2022 na 2023, ukuaji wa mikopo ulifikia wastani wa asilimia 19.8 ikilinganishwa na asilimia 6.6 katika miaka miwili iliyotangulia.

MJUE MWENDESHA BOTI BI. BAHATI ISSA....

# Kukerwa na manyanyaso lifti akajifunza, leo nahodha, mwongoza watalii mahiri

- Anuia kumiliki chake, kinamama wamhusudu balaa
- Staili yake anawavusha wageni visiwani, kuwapikia

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

HAIKUWA kazi nyepesi kwangu kuingia baharini peke yangu mwanamke na kuwa Nahodha na kuchukua chombo na kuanza kuzunguka nacho baharini, bila ya mwanaume," anatamka Nahodha wa chombo cha majini, Bahati Issa (51).

Anaendelea: "Lakini kwa sababu wanawake huwa tunaamini hakuna tusichokiweza na tukiamua jambo, huwa tunalikamia sana, ili basi na mimi nikasema nitaweza na nikaingia mzigoni."

Bahati anaisimulia Nipashe, akiwa katika Pwani ya Unguja, kwamba wasifu wake kifamilia ni mama wa watoto sita, ameolewa na mume Khamis Hassan Haji, kazini akiendesha chombo cha baharini kiitwacho Nipe Tano, jina linalobeba tafsiri hitaji la kuungwa mkono.

Bahati anaangukia orodha ya wanawake walio na uthubutu wa kusafirisha watalii kutoka endo maarufu kijiji cha Kikungwi, mkoa wa Kusini Unguja

Akiwa na boti yenye mashine ya kisasa kutoka, wakisafiri hadi katika visiwa maalum vyenye uwekezaji mkubwa, ikiwamo Nyemembe, Miwi, Komonda, Kwale na Punguze.

Ni safari za visiwani zinazochukua mwendo baharini wastani wa dakika 30 hadi dakika 60, kutegemea na umbali wa killipo na huwa anajikita huko, akitumikia unahodha wake.

Anataja siri ya kuhama kitaaluma eneo hilo, ni kwamba, baada ya kuona wanaume wamejikita peke yao katika kazi hiyo, akitaja sababu kwamba:.

"Baada ya kuona shughuli hizi zinafanywa na wanaume peke yao kijijini hapa, wakati wanawake na sisi tuna fursa ya kufanya kazi hii.

"Na baada ya kuingia nimekubalika na nimeaminika maana baadhi ya watalii hawaridhiki mpaka niwasafirishe mimi na wamenipachika jina la Mama Afrika," anasimulia.

Bahati anasema,baada ya kuwafikisha watalii visiwani, pia anawahudumia kwa kuwaandalia chakula, ambapo kawaida baada ya kuogolea, huhitaji mlo kabla ya kuwarudisha katika eneo la awali.

Akieleza mafanikio aliyoyapata kutokana na kazi hiyo, amemudu kujenga nyumba ya makazi anakoishi, anawasomesha watoto wake shule, pia amenunua chombo cha usafiri bodaboda kwa ajili ya biashara.

Sasa bahati anatoa rai, kwamba wanawake wenzake kujitoa bila ya kuchagua kazi na upungufu wa kijinsia iwe pingamizi ya wanawake kufanya kazi za kujikwamua kiuchumi na kupata kipato.

**ALIKOKUWA ZAMANI**

Anataja awali kabla ya kazi hiyo ya unahodha, alijishughulisha na a uvuvi wa chaza akiwa na wanawake wenzake kijijini hapo, ndipo akaanza kujifunza unahodha kwa sababu ya kunyanyasika wakati wakihitaji usafiri wa mashua baharini kwa ajili ya shughuli hiyo ya uvuvi wa chaza.

"Baadhi ya manahodha wanaume wakitukejeli kwa maneno ya kutuvunja moyo, wakati tunahitaji usafiri wakituambia kuwa katika chombo hatupakii wanawake.




Nahodha Bahati Issa, akiwa 'chomboni'. **PICHA; RAHMA SULEIMAN**

"Kama mnaweza kuendesha chukuweni chombo muendele, tukakaa kwa Pamoja, tukasema madhila haya yatatukumba mpaka? Hebu tujitokezeni tujifunze sisi wanawake kuendesha," anasimulia chimbuko lake.

Hapo anasimulia wakajitokeza baadhi ya wanaume kuwafundisha na yeye akawa pekee aliyejitokeza kujifunza, leo hii sasa kawa mjuzi wa uendeshaji chombo cha usafiri baharini jasiri na asiye na woga majini.

Nahodha huyo mwanamke anasema kabla ya kujikita kusafirisha watalii, akawa anawasafirisha wanawake wenzake wavuvi wa chaza, kutoka sehemu moja kwenda kwingine baharini, kwa ajili ya uvuvi huo.

"Tangu nianze kuendesha chombo hiki cha baharini inafika miaka 20, lakini kwa kusafirisha watalii visiwani kwa sasa nina muda wa miaka mitano" anasimulia Nahodha Bahati.

**SURA YA CHANGAMOTO**

Kuhusu changamoto ya kazi yake, anataja kuwapo wakati mwingine mashine ya mashua huharibika wakiwa safarini katikati baharini na wageni huwa hawaamini kufkishwa salama, pia changamoto ya 'Upepo wa Kusi na Kaskazi...' anasema

Nahodha huyo anasema, matarajio yake baadaye ni kumiliki mashua yake, kwani anayofanyia kazi sasa sasa ni ya kukodi, hivyo kipato cha hukigawanya na mmiliki.

Hata hivyo, yu katika hatia amekuwa gumzo kwa baadhi ya wanawake kijijini anakotoka, wakimuelezea kuwa mwanamke jasiri na asiyeogopa madhila ya baharini, hasa wakimhsudu anavyoendesha boti hilo kwa ufanisi, akisafirisha wageni wake watalii.

"Sisi ni wanawake, lakini hatuna ujasiri kama wake wa kuingia majini na kuendesha chombo cha bahari kama yeye. Lakini, tunamhusudu na tunamuombea kwa Mungu ampe nguvu na kumuongezea ujasiri.

"Maana angekuwa na hofu kama sisi wengine, asingeweza 'kuteremesha' chombo na angetetemeka akashindwa njiani. Lakini, tunamsifu sana yeye ni Hodari!" anatamka mwanamke anayejitambulisha jirani yake wa karibu, pasipo kufafanua jina lake.

Sheha (Katibu Kata) wa Shehia ya Kikungwi, Muhammed Haji Ushahidi, anamtaja Bahati mwanamke wa mfano katika kijiji hicho, hata kimaendeleo anawasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Bi Bahati ni jasiri! Ni mwanamke anayejiamini, mwanamke anaepambana kutafuta maisha, ni mwanamke anayejielewa, kwa sababu 'wanawake 'wanaweza wakiwezeshwa', lakini wapo wanawake ambao wanaogopa kujitoa, niwaombe wajifunze kwa Bi Bahati jinsi anavyojitoa," anasema.

Sheha huyo, anamsifu kwamba ni wa kujitoa na nguzo kubwa kijijini kwake, maana licha ya kuendesha boti, pia ana kazi ya kuhudumia watalii visiwani, akionekana anafaa kwa ufanisi.

Anawafafanua, wanawake kijijini aliko wamegawanyika kwenye makundi, katika nyendo zao za kutafuta kipato, wapo waliojikita katika uvuvi wa samaki chaza.

**DARASA LA UNAHODHA**

Khamis Juma Mwalimu ni mwalimu wa Bahati kuendesha boti, anasema mwanafunzi wake huyo sasa ni mvuto wa wageni, wengi wapofika hapo hupendelea kusafirishwa na Bahati.

"Huyu Mama ni mwanafunzi wangu, kwa kweli ni mwanamke hodari, anayejituma na wala haoni aibu katika kufanya kazi yoyote ya kujipatia kipato," anasema.

Ni hoja inayopokewa na Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Dk. Tumaini Gurumo, anayesema ushiriki wa wanawake katika masuala ya bahari sio mkubwa, wengi wamejikita katika usajili wa usafirishaji wa meli.

Dk. Gurumo anaeleza kwamba, katika nafasi ya ubaharia, bado idadi ni ndogo na kuna kazi kubwa ya kuwashawishi wakijikite katika nafasi hiyo.

Hata hivyo, anawatoa hofi kwamba, nafasi ya ajira baharini hazitazami jinsia, kwani hata sheria za kimataifa zimebadilika, zikimpa nafasi mwanamke kuingia baharini na kupata haki anazostahili, sawa na mwanaume.

Anataja mzizi wa kasoro ulioko sasa inatofautiana na zamani, kuwa 'mtoto wa kike hawezi kufanya kazi za baharini'. Anasisitiza, mtazamo huo wa kale uliwazibia fursa na lazima wanawake sasa wapewe nafasi kujikwamua, familia zao na taifa kwa ujumla.

Kisiwa cha Zanzibar kina ajira nyingi za baharini, hivyo ili nchi kuendelea kutoweka mipaka baina ya wasichana na wavulana lazima wote kuwapa nafasi kuingia katika fani hizo na kusaidia nchi na jamii.

"Wapo wasichana tuliowafundisha sasa ni manahodha na wahandisi kwenye Meli kwa hivyo sio neo la kusema ni tambuu kama zamani hivi sasa milango ipo wazi, teknolojia imekuwa hakuna meli itakayozunguka kukaa baharini kwa muda mrefu kutoka bandari moja kwenda nyengine, hivyo ipo nafasi kwa wasichana"alisema Dk Gurumo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanawake wameonyesha uwezo, juhudi za ziada zinatakiwa sasa

**WANAWAKE** nchini Tanzania leo wanasherehekea Siku ya Wanawake Duniani ikiwa ni kumbukumbu ya harakati zao katika kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kijamii pamoja na kupata haki sawa katika maeneo mbalimbali.

Siku hii husherehekewa kwa namna tofauti kwenye mataifa mbalimbali duniani kwa lengo la kuwaweka pamoja wanawake katika kudai haki zao na kubadilishana uzoefu juu ya mafanikio katika harakati zao za usawa katika umiliki mali, uongozi na ushiriki katika ngazi za uamuzi.

Katika kuonyesha kuwa wanawake wana nafasi kubwa katika jamii, kumekuwa na misemo mbalimbali inayowatambulisha kama vile 'Wanawake jeshi kubwa', 'Wanawake wakiwezeshwa wanaweza' na palipo na mafanikio ya mwanamume nyuma yuko mwanamke'. Yote hiyo ni kuonyesha nafasi aliyo nayo mwanamke katika maendeleo kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Siku ya Wanawake Duniani ina historia ndefu tangu mwaka 1908 baada ya wanawake 15,000 walioandamana New York, Marekani wakidai kupunguziwa muda wa kufanya kazi, ujira wa kuridhisha na haki ya kupiga kura. Maandamano hayo yalizaa matunda kwani kwa mwaka mmoja baadaye ilitangazwa rasmi kuwa siku ya kitaifa kwa wanawake na mwaka 1910, mwanamama Clara Zetkin alianzisha wazo la kuwa na siku ya kimataifa ya wanawake.

Tangu wakati huo, kumekuwa na mafanikio makubwa katika ushirikishwaji wa wanawake kutokana na mambo ya kiusawa waliyoyaomba katika nchi zao kutokana na hali halisi iliyokuwako kwa nyakati tofauti. Katika baadhi ya mataifa, mpaka miaka michache karibuni, wanawake walikuwa hawaruhusiwi hata kupiga kura lakini kutokana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea duniani, mambo yamebadilika kwa kiasi kikubwa.

Aidha, masuala ya wanawake yameingizwa katika mikataba na itifaki za taasisi za kimataifa msisitizo mkubwa ukiwa kupewa nafasi sawa na wanaume hususan katika ngazi za uamuzi. Katika baadhi ya jumuiya za kikanda kama vile Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) suala la wanawake limewekwa wazi kuhusu uwiano wa kijinsia hususan katika uongozi. Mkazo umewekwa kuwa na uwiano wa 50:50 wa nafasi katika vyombo vya uamuzi.

Kutokana na itifaki hizo, imeshuhudiwa katika nchi nyingi wanawake wamepewa nafasi na fursa kubwa katika masuala ya maendeleo, siasa na uongozi katika sekta na taasisi mbalimbali. Nchini Tanzania, kwa mfano, kiongozi wa juu kabisa, kwa maana ya Rais, ni mwanamke na pia wako wanawake katika nafasi mbalimbali kama vile mawaziri, makatibu wakuu, wakuu wa mikoa na wilaya pamoja na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa.


Pia wako majaji wanawake katika mahakama kuu na mahakama ya rufani pamoja na mahakimu ambao wameonyesha uwezo mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yao. Hata katika taasisi za kifedha, wako wanawake ambao wengine walishakuwa manaibu gavana, maofisa watendaji wakuu na wakurugenzi wa idara mbalimbali ambao wamefanya mambo makubwa na kusababisha taasisi wanazoziongoza kupata heshima kitaifa na kimataifa.

Vyombo vya Habari pia haviko nyuma katika kuwapa wanawake nafasi za uongozi kwa kuwa wako maofisa watendaji wakuu, wahariri wakuu na watendaji sambamba na wakuu wa vitengo ambao kwa hakika nao wamefanya mambo makubwa katika taasisi walizopewa kuziongoza pamoja na nafasi walizoaminiwa kuzitumikia.

Ni ukweli kwamba wanawake waliopewa nafasi za uongozi katika taasisi za umma, binafsi, mashirika ya kimataifa na ngazi za uamuzi, wameonyesha uwezo mkubwa katika utendaji wao. Pamoja na ukweli huo, jitihada zaidi zinapaswa kufanyika ili kuhakikisha mazuri yaliyofanywa na kundi hilo yanaendelezwa na kizazi kijacho hasa vijana na watoto wa sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hizi ndizo sifa za huyo mwanamke tunayeadhimisha siku yake leo

**LEO** ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yenye mzizi wa mwaka 1908, baada ya jitihada za wanawake 15,000 walipoandamana mjini New York Marekani kudai kupunguziwa muda wa kufanya kazi, ujira wa kuridhisha na haki ya kupiga kura.

Kuwapo kwa maadhimisho ya siku hiyo, kuwapo mambo mengi ambayo wanawake wamekuwa wakiyalilia, hasa suala la uwiano sawa kati yao na wanaume kwenye ngazi za maamuzi na hata katika uongozi.

Wakati leo ikiwa ni kilele cha maadhimisho hayo, ninadhani kuna haja ya kukumbusha mambo kadhaa kuhusu mwanamke ili kuondoa dhana potofu ambayo imejengwa dhidi ya kutokana na mila na desturi.

Mwanamke ana sifa nyingi kuanzia upole, usikivu, subira, kubeba majukumu makubwa. Yeye ni sehemu ya jamii, kwani siku zote kuwe na sherehe, misiba au mtoto kuumwa, huwa yuko mstari wa mbele.

Vilevile, uamuzi wa mwanamke huwa hauna haraka, hutanguliwa na tafakari kabla ya kuchukua hatua kwa lengo la kutoa uamuzi makini na wenye manufaa nyumbani, katika jamii au hata sehemu ya kazi.

Lakini kabla ya kuendelea, kuna haja ya kufafanua zaidi kuhusu mwanamke, kwamba nafasi yake katika familia na kwa jamii hasa katika dunia ya leo ambayo imeamua kutambua umuhimu wake.

Ukweli ni kwamba, mwanamke ni nguzo, muhimu na mlezi katika familia, kwani amekuwa muhimu hasa pale mwanaume anaposhindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ndani ya familia.

Sio siri kwamba, kwa nyakati tofauti mwanamke anapambana kuhudumia familia kuhangaika kule na kule kuhakikisha watoto wanapata chakula, hayuko tayari kuona watoto wanateseka. Ninaamini kuna watu wengi ambao wameshuhudia jinsi ambavyo mwanamke amekuwa akipambania familia, hasa watoto bila kukata tamaa pale mzazi mwenzake anapotelekeza familia.

Sioni haya kusema kwamba mwanamke ni msingi ndani ya familia katika nyanja mbalimbali, kwani ninaamini kuwa mwanaume akitoa maamuzi au amri, mwanamke anakuwa msingi wa maamuzi na utekelezaji.

Maana yangu ni kwamba, mwanamke huleta maamuzi chanya ndani ya familia ambayo huifanya iweze kusimama imara na kuwa na umoja badala ya kusambaratika. Huyo ndiye mwanamke.

Mwanaume ni mtu wa kutoa amri au kupitisha sheria bila kuangalia madhara yake kwa familia, lakini kwa kuwa mwanamke ana sifa ya usikivu na subira, huwa ni rahisi kwake kutoa uamuzi sahihi. Ukiangalia nafasi mbalimbali za mwanamke katika jamii, utagundua umuhimu wake ni mkubwa iwe ni wake katika shughuli za uzalishaji mali kuanzia kwenye kilimo na hata biashara ndogo na kubwa.

Vilevile, mwanamke huwa anapenda maendeleo katika familia. Kwa lugha nyingine ni kwamba ana wivu wa maendeleo, ndio maana wako tayari kubembeleza na kushawishi waume zao jambo la kufanya kwa ajili ya maendeleo ya familia. Hivyo, umuhimu wao si wa kubeza.

Katika dunia ya leo, mwanamke anaendelea kupambana ili kuondoa dhana kwamba kuna kazi ya mwanamke na mwanaume, badala yake kazi wanazofanya wanaume na wao sasa wanazifanya tena kwa ufanisi.

Hatua hiyo ya wanawake kuonyesha uwezo wao katika majukumu mbalimbali, imeondoa mawazo na mila potofu ambayo awali ilijenga na kusababisha wawe nyuma katika ngazi za maamuzi.

Ongezeko la wanawake katika ngazi za maamuzi, imekuwa chachu na kuwafanya wengine zaidi kuibuka katika nafasi mbalimbali za kazi na uongozi na kuonyesha umahiri mkubwa katika utendaji.

Hivyo, maadhimisho haya yawe ni chachu ya kuendelea kuwainua wanawake ili hatimaye wafikie lengo walilokusudia la kuwa na uwiano wa uongozi na katika ngazi za maamuzi 50 kwa 50.

# Mloganzila kurekebisha wenye macho makengeza

**Na Joseph Mwendapole**

NDOTO za kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii tiba nchini zinaendelea kutimia baada ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Mloganzila kuandaa kambi ya siku tano ya upasuaji rekebishi wa macho.

Kambi hiyo inatarajiwa kuanza Machi 11 hadi 15 katika hospitali hiyo, jijini Dar es Salaam.

Msemaji wa Global Medicare ambao ndiyo waratibu wa kambi hiyo, Albert Kilalah, alisema kambi hiyo inawahusu watu wenye makengeza, kope zinazoshindwa kufunguka na wenye makovu ya ajali.

Alisema kambi hiyo itaendeshwa na madaktari bobezi kutoka nje ya nchi ambao ni Dk. Nabila Elias na Dk. Safwat El badri kutoka Dubai.

"Wenye changamoto zilizotajwa hapo juu wakipata taarifa hizi wafike Mlonganzila kwaajili ya kufanyiwa vipimo vya awali kabla ya kuanza kwa kambi hiyo siku ya Jumatatu tarehe 11 hii ni fursa nzuri ya kukutana na madaktari bingwa kwa hiyo waitumie," alisema.

Alisema madaktari hao watashirikiana na bingwa wazawa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Mlonganzila.

Pia, ili kubakiza ujuzi huo nchini wamealikwa madaktari kutoka hospitali za Benjamin Mkapa Dodoma, Hospitali ya Kanda Mbeya, Bugando Mwanza, Tumbi Kibaha, Hospitali ya Mtwara RRH pamoja na CCBRT ya Msasani, Dar es Salaam.

"Hawa madaktari wazawa watashirikiana na madaktari bingwa kutoka Dubai kufanya upasuaji huu fursa ambayo wataitumia kama sehemu ya kujifunza ili wageni watakapoondoka wazawa wawe wanaendelea kufanya upasuaji wa aina hii," alisema.

Alisema kambi hiyo inakuja kutokana na uwekezaji mkubwa wa vifaa tiba vilivyonunuliwa na serikali ya awamu ya sita sambamba na madaktari kusomeshwa kwa wingi na kupewa utaalamu wa hali ya juu kufanya matibabu ya kibingwa.

Alisema zamani matibabu kama hayo yalikuwa yakifanyika nje ya nchi, lakini kutokana na uwekezaji huo yanafanyika nchini.

"Zamani wagonjwa kama hawa tuliwapeleka nje ya nchi, lakini sasa madaktati bingwa kutoka nje wanakuja kuwatibu wagonjwa wetu hapahapa kwasababu nchi ina kila aina ya vifaa tiba ambavyo tulikuwa tunalazimika kuvifuata nje ya nchi na kwa sasa nchi ina madaktari bingwa wenye uwezo mkubwa wa kutumia vifaa hivyo," alisema.

Daktari bingwa wa macho wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Pwani Tumbi, Fadhili Swai, alisema anafurahi kuona wanakwenda kutoa huduma ambayo ni nadra sana kufanywa hapa nchini.

"Natoa rai kwa Watanzania wazitumie siku hizo tano kwasababu hiyo ni huduma ya kipekee na adimu sana kutokea nchini. Wanapokuja madaktari bingwa kutoka nchi mbalimbali tunabadilishana ujuzi na mbinu za tiba kwa hiyo hii ni hatua muhimu sana kwetu," alisema.

Daktari bingwa wa macho wa Hospitali ya RRH Mtwara, Mganga Majura, alisema ujio wa madaktari hao unakwenda kutambulisha hospitali za Tanzania kimataifa kwa kuwa baadhi ya Watanzania wageni hawajui uwekezaji mkubwa kwenye afya ya macho uliofanywa katika Hospitali ya Muhimbili.

"Hii ni fursa ya kutambulika duniani na tukiwa na madaktari hawa watalii wanaokuja nchini watakuwa na imani kwamba hata wakiugua macho watapata matibabu ya kitaalamu kama ambayo wangepata wakienda nchi zilizoendelea," alisema.

Alisema kambi hiyo itawasaidia madaktari wa ndani na wageni kupeana mbinu mpya za tiba ya kibingwa ya macho na baadaye kufanyika kwenye hospitali za mikoa mbalimbali bila kulazimika kwenda Muhimbili.




Mkurugenzi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT), James Mbalwe akizungumza kwenye mkutano na wahariri na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na bodi hiyo tangu kuanzishwa kwake. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbowe akimbilia mahakamani kuzuia nyumba kupigwa mnada

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe amekimbilia Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kuinusuru nyumba iliyokamatwa kwa amri ya mahakama ili kulipa Sh. milioni 62.7 za mishahara ya waandishi wa habari 10 wanaomdai mtoto wake, Dudley Mbowe, ambaye ni Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima.

Mbowe kupitia wakili wake, John Mallya aliwasilisha shauri hilo chini ya hati ya dharura mbele ya Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Mary Mrio.

Alifungua shauri dhidi ya Maregesi Paul, Fidelis Felix, Christina Mwakangale, Janeth Josiah, Exuperius Kachenje, Hellen Sisya, Kulwa Mzee, Nora Damian, Makuburi Ally, Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania na Kampuni ya Udalali ya JJ Auctioneers& Debt Collectors.

Wakili Mallya alidai, wajibu maombi tayari wamepewa madai yao pamoja na hati ya kiapo iliyoapwa na Mbowe Februari 26, mwaka huu.

"Mheshimiwa wajibu maombi tumeshawapa nakala hivi karibuni tusikilize kama wamekuja na majibu," alidai Mallya.

Akijibu hoja hizo, mmoja wa wajibu maombi, Kulwa Mzee, alidai ni kweli wamepokea nyaraka hizo, zikiwa zimeambatanishwa na hati ya kiapo iliyoapwa na Mbowe, akiomba nyumba iachiliwe, na Mahakama itoe amri wajibu maombi wamlipe gharama kutokana na utekelezaji wa amri hiyo.

"Mheshimiwa tumepitia nyaraka wenzetu wametupa siku 15 tujibu, tunaihakikishia Mahakama kwamba tutajibu ndani ya muda tuliopewa," alidai Kulwa.

Wakili Mallya akijibu hoja hiyo, alidai shauri lao wameliwasilisha chini ya hati ya dharura, maombi yao ni kuiondoa nyumba hiyo kwa kuwa tayari ilishabandikwa matangazo kwa ajili ya kupigwa mnada.

Alidai ikiendelea kuwa kama ilivyo inaweza kupigwa mnada kwa sababu suala hilo lina muda wa utekelezaji.

Akijibu, Kulwa alidai ni kweli maombi yapo katika hati ya dharura, lakini lazima wasome vizuri ili wajibu kwa kuwasilisha hati ya kiapo kinzani kwa sababu katika maombi hayo kuna suala la kumlipa mwombaji gharama.

Aliomba kama siku 15 nyingi watajibu ndani ya siku saba, Mahakama ilikubali majibu yawasilishwe mapema, shauri hilo litasikilizwa Machi 12, mwaka huu. Mbowe anadai nyumba hiyo iliyokamatwa si mali ya Dudley na kwa kuthibitisha hilo ameambatanisha hati ya nyumba hiyo yenye jina la Freeman Mbowe.

Mahakama hiyo pia imepanga kuendelea na shauri la madai ya waandishi hao kwa Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley, Machi 12, mwaka huu.

Februari 13, mwaka huu, Mahakama ilikubali maombi ya wadai na kumteua dalali wa Mahakama kukamata nyumba kwa ajili ya kuipiga mnada.

Februari 28, mwaka huu, dalali wa Mahakama, Jesca Massawe, alifanikiwa kubandika matangazo ya kukamata nyumba ya Mkurugenzi tayari kupigwa mnada kufidia deni la malimbikizo ya mishahara wafanyakazi.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Mary Mrio alitoa amri hiyo baada ya kupitia hoja za washinda tuzo katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Julai 2023.

Shauri hilo namba 28461 la mwaka 2023, wadai ni Maregesi Paul na wenzake tisa dhidi ya Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley Mbowe.

Baada ya mdaiwa kukaidi kulipa, wadai walikubaliana njia sahihi kukamata nyumba yake namba 9 iliyopo Mtaa wa Feza, Mikocheni B, Barabara ya Chipaka na Mahakama ilikubali. Walalamikaji hao walipata tuzo Julai 17, 2023 mbele ya Msuluhishi wa CMA Ilala, Bonasia Mollel.

Madai ya awali yalikuwa jumla ya Sh milioni 114 baada ya kukaa mezani kwenye majadiliano kwa pamoja kiwango hicho cha fedha kilishuka na kufikia Sh milioni 62.7.

Dudley alikubali kulipa fedha hizo kwa awamu tatu, Oktoba 30 hadi Desemba 30, 2023 na awamu ya mwisho ilikuwa mwishoni Februari, mwaka huu lakini hakulipa.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Wadau duniani wavutiwa kuwekeza Tanzania sekta utalii

**Na Mwandishi Wetu,**
BERLIN

KAMPUNI kubwa zinazojishughulisha na masuala ya utalii duniani zimevutiwa kuwekeza Tanzania katika huduma za malazi, usafirishaji na utangazaji wa sekta hiyo.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, alisema hayo katika Maonesho ya Utalii ya ITB yanayoendelea jijini Berlin, Ujerumani.

"Nimefurahi kukutana na kampuni kubwa ya TUI (TUI Group) yenye makao makuu nchini Ujerumani ambayo ina hoteli zaidi ya 400 duniani, meli za kitalii 16, mashirika ya ndege matano na zaidi mashirika 1,200 ya usafiri," alisema.

Alifafanua kuwa kampuni hiyo imewekeza Zanzibar na hadi kufikia Juni, mwaka huu itazindua hoteli yao ya tisa na kwa upande wa Tanzania bara inaendelea kufungua safari za ndege ili kuleta watalii katika hifadhi zilizopo nchini.

Aidha, Kairuki amekutana na kampuni inayosafirisha watalii zaidi ya milioni 1.2 duniani yenye Makao Makuu Marekani na Puerto Rico ambayo imeonyesha utayari ifikapo Mei, mwaka huu italeta wakala wa usafirishaji zaidi ya 40 kutembelea maeneo mbalimbali Tanzania.

Waziri Kairuki pia amekutana na kufanya mazungumzo na kampuni ya kimataifa kusafirisha watalii ya Expedia Group na kampuni kutoka Slovakia ambayo inapeleka watalii duniani kwa zaidi ya asilimia 85 kutoka nchini humo na ina matangazo katika runinga zao na kujadili namna ya kushirikiana katika kuandaa matangazo ya vivutio vya utalii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Damas Mfugale, alisema ushiriki wa Tanzania kwenye maonesho hayo ni chachu ya kuongeza idadi ya watalii nchini.



Ofisa Mawasiliano wa Barrick, Neema Ndossi (wa tatu kulia), akikabidhi msaada wa mashine ya kupima mwenendo wa mgonjwa (Patient Monitor) kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala, Dk. Zavery Benella katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Dar es Salaam jana. Wengine ni wafanyakazi wa Barrick alioongozana nao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadaiwa kupokea hongo ununuzi vifaa ujenzi wa shule

**Na Joctan Ngelly,**
BIHARAMULO

WAFANYAKAZI watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo na wazabuni wawili wamepandishwa kizimbani Mahakama ya Wilaya ya Biharamulo, mkoani Kagera kwa makosa ya kutoa na kupokea hongo ya Sh. 3,278,700 katika ununuzi wa vifaa vya umeme kwenye ujenzi wa Shule ya Msingi Kikomakoma mpya.

Washtakiwa hao ni Hauson Reverian (43) ambaye ni Ofisa Elimu Takwimu na Vifaa, Thobias Mganga (44), Mkuu wa Shule ya Msingi Kikomakoma mpya, Gloria Kajuna (36), Mkaguzi, Salanga Mayenga (48), Mzabuni na Vedasto Kiporoka (49), Mzabuni, wote wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera.

Washtakiwa wote walipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi, Subira Mashambo, hata hivyo walikana kuhusika na makosa hayo.

Hakimu Mashambo alisema washtakiwa watatu, Gloria, Salanga na Vedasto watakuwa nje kwa dhamana.

Pia, Hakimu Mashambo alisema washtakiwa wawili ambao ni Hauson na Thobias, watakuwa mahabusu kwa kukosa wadhamini.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera, Kelvin Murusuri, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali (PH).

Hakimu Mashambo alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Machi 12, mwaka huu kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali (PH).

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili Kiongozi wa TAKUKURU Mkoa wa Kagera, Murusuri alidai kuwa kati ya Mei na Juni, 2023 washtakiwa wote kwa pamoja walijipatia manufaa ya kutoa na kupokea hongo ya Sh. 3,278,700 katika ununuzi wa vifaa vya umeme kwenye ujenzi wa Shule ya Msingi Kikomakoma mpya na kushitakiwa kwa makosa ya kutoa na kupokea hongo kinyume na kifungu cha 15(1)(a) na (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329 Marejeo ya mwaka 2022.

Aidha Murusuri alisema katika kosa la pili washitakiwa walihadaa katika malipo kinyume na kifungu cha 304 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 Mapitio ya mwaka 2022 kwa kulipa wazabuni tajwa Sh. 23,414,000 ambayo ni zaidi ya stahiki yao katika ununuzi uliofanywa kwa lengo la kujipatia fedha hizo toka kwa wazabuni hao.

# Kortini tuhuma za kusafirisha sukari, mafuta kimagendo

**Na Grace Gurisha**

VIJANA saba wakazi wa Kunduchi, jijini Dar es Salaam, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, wakikabiliwa na mashitaka manne likiwamo la kusafirisha sukari na mafuta ya kupikia zaidi ya madumu 100 kwa njia ya magendo kupitia bandari bubu kutoka nje ya Tanzania.

Vijana hao ni mfanyabiashara Mustapha Bakari (30), mkazi wa Kunduchi, mafundi Mohamed Nassor (25) na Abdulmajid Kheri (17), dereva Erick Solomon Mwagemba (25), dereva Justin Mollel (35), pamoja na wavuvi Mbaraka Mwanjovu (23) na Hamad Hamad, maarufu Katoto (23).

Washitakiwa hao walisomewa mashitaka yao kwa mahakimu watatu tofauti ambao ni Hakimu Mkazi Mwandamizi, Veneranda Kaseko, Mahakimu Wakazi, Nabwike Mbaba na Ramadhani Rugemalira wa mahakama hiyo.

Akisoma hati ya mashitaka jana mbele ya Hakimu Mbaba, Wakili wa Serikali, Auni Chilamula, alidai kuwa washitakiwa Nassoro na Kheri wanadaiwa Februari 11, 2024 wakiwa eneo la Kunduchi, wilaya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, walikutwa wakiingiza mifuko 20 ya sukari kwa kutumia njia ya magendo hivyo kukwepa ushuru wa Sh. milioni 2.3.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe na mahali hapo, washitakiwa hao walikwepa ushuru kwa kuingiza mifuko 20 ya sukari kwa kutumia gari lenye namba za usajili T 956 BBF kinyume na sheria.

Chilamula alidai kuwa washitakiwa hao walishindwa kuwasilisha nyaraka za bidhaa za magendo.

Mbele ya Hakimu Kaseko, Erick anadaiwa tarehe na mahali hapo, mkoani Dar es Salaam, alisafirisha mifuko 20 ya sukari kupitia bandari bubu na kukwepa ushuru wa Sh. milioni 2.3.

Mbele ya Hakimu Rugemalira, washitakiwa Mollel, Mwanjovu na Hamad, wanadaiwa Februari 11, 2024 maeneo ya Mtongani-Kunduchi, walisafirisha madumu 100 ya mafuta ya kupikia kupitia bandari bubu na kusababisha ukwepaji wa ushuru wa Sh. 4,022,113.

Bakari anadaiwa kuwa Februari 11, 2024 maeneo ya Mtongani Kunduchi, wilayani Kinondoni, kinyume na sheria aliingiza madumu 50 ya mafuta ya kupikia kupitia bandari bubu na kusababisha ukwepaji wa ushuru wa zaidi ya Sh. 2,000,000.

Inadaiwa Februari 11, 2024, maeneo ya Mtongani Kunduchi, Bakari akiwa dereva wa gari lenye namba za usajili T 964 DPJ aina ya Toyota Bravis, alisafirisha madumu 50 ya mafuta ya kupikia yaliyotoka nje ya Tanzania.

Pia, inadaiwa katika tarehe na mahali hapo, Bakari alishindwa kuandaa taarifa ya usafirishaji wa madumu 50 ya mafuta ya kupikia huku akijua kuwa hiyo ni bidhaa hazijalipiwa na kusababisha kukwepa kodi ya Sh. 2,011,057.

Inadaiwa Bakari akiwa msimamizi na dereva wa gari lenye namba za usajili T 964 DPJ aina ya Toyota Bravis, kinyume na sheria alikutwa akisafirisha madumu 50 za mafuta ya kula yaliyokuwa yakitoka nje ya Tanzania huku akifahamu kuwa ni bidhaa ni za magendo.

Washitakiwa hao hawakuruhusiwa kujibu tuhuma hizo, upande wa mashitaka ulidai kuwa upelelezi bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Machi 21, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.



# Ummy apiga marufuku kuficha takwimu vifo vya watoto

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema kuanzia sasa hataki kusikia sababu za waganga wakuu wa mikoa na wilaya nchini kuficha takwimu za vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Badala yake, ameagiza watoe takwimu sahihi za vifo hivyo, pamoja na vile vya watoto walioko chini ya mwaka mmoja pamoja na vifo vya watoto wachanga wenye umri wa chini ya siku 28.

Ummy alitoa agizo hilo jana jijini Tanga alipokutana na wakufunzi 110 kutoka vituo 25 vinavyotoa huduma ya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni (CEMONC).

Vituo hivyo huchangia asilimia 86 ya wajawazito wanaojifungua katika vituo 44 vya Mkoa wa Tanga.

"Dhamira ya serikali ni kuhakikisha inaokoa maisha ya wanawake na watoto wachanga.

Rais Samia Suluhu Hassan, anataka kuona takwimu za makundi hayo matatu pamoja na takwimu za kinamama wajawazito.

Aidha alisema ni muhimu kuendelea kutoa mafunzo kazini kwa watoa huduma za afya kwa kuwa taarifa zinaonyesha kuwa kati ya vifo 100 vitokanavyo na uzazi vinavyotokea, asilimia 85 ya vifo hivyo vina uhusiano na mapungufu ya ujuzi.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto wa Wizara ya Afya, Dk. Felix Bundala, alisema hadi kufikia Juni mwaka 2025, serikali imepanga kuwafikia wakufunzi 2,860 katika mikoa yote 26 ili waweze kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi mama na mtoto.



Mteule wa nafasi ya Udiwani kata ya Mkuzi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), George Chambai (kulia), akirudisha fomu kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa kata hiyo, Idd Rwanjoro, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# NCCA, wafugaji wakutana, waelimishana kuhusu hifadhi

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

KAMISHNA wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Richard Kiiza, amefanya mazungumzo na wafugaji wa jamii ya kimasai waliopo ndani ya hifadhi hiyo, huku akiwaeleza kuwa serikali hailazimishi mtu kuhama, isipokuwa inaelimisha hasara za kuishi ndani ya hifadhi.

Kiiza alikutana na wafugaji hao jana katika vijiji vya Kayapusi na Oloirobi vilivyoko Kata ya Ngorongoro alipokwenda kukagua maendeleo ya timu ya uelimishaji na uandikishaji wa wananchi wanaotaka kuhama kwa hiari ndani ya hifadhi hiyo.

"Unajua sheria inazuia kufanya baadhi ya vitu ukilinganisha na mazingira anakoenda. Sasa, serikali imeboresha mazingira kwa kujenga miundombinu ya maji, shule, barabara, umeme, mawasiliano, eneo la malisho, minada na soko la maziwa," alisema.

Wananchi wanaohama kwa hiari katika eneo hilo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wanakwenda kuanza maisha mapya katika Kijiji cha Msomera kilichoko Kata ya Misima, Wilaya ya Handeni na mkoani Tanga.

Maeneo mengine yaliyotengwa na serikali kwa ajili ya wanaohama kwa hiari Ngorongoro ni Kijiji cha Kitwai kilichoko Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara na Kijiji cha Saunyi, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga.

"Wananchi ambao wanapenda kwenda kuona maeneo yaliyoandiliwa na serikali kabla ya kuamua kuhamia huko wana uhuru wa kufanya hivyo, ili kukagua maeneo yaliyoandaliwa na serikali ipo tayari kuwapa ushirikiano.

"Serikali haiwezi kuwa na nia mbaya kwa watu wake, ndiyo maana inajenga miundombinu yote muhimu, inawapa wananchi wanaohama fedha za motisha zinazotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Pamoja na kuwapa fidia ya maendelezo waliyofanya wakiwa ndani ya hifadhi na kuwahamishia thamani na mifugo yao yote kwenda maeneo waliyochagua, kwa kufuata misingi ya sheria, kanuni na haki za binadamu."

# TANROADS yatumia bil.5/- kukarabati miundombinu Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MVUA za El-Nino zimesababisha hasara na uharibifu wa miundombinu ya barabara katika Mkoa wa Kilimanjaro, jambo ambalo limeisukuma Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), kutumia zaidi ya Sh. bilioni tano kwa ajili ya kukabiliana na madhara hayo.

Jana, Meneja wa TANROADS mkoani humo, Motta Kyando, alisema fedha hizo zimetumika kurejesha mawasiliano ya barabara kwa kujenga upya madaraja mbalimbali, likiwamo la Daraja la Biriri lililoko eneo la kwa Wasomali Wilaya ya Siha.

Alisema daraja hilo limekuwa na desturi ya kufurika maji wakati wa msimu mvua na kisha kukata mawasiliano katika Barabara Kuu ya Moshi/Arusha. Daraja hilo limejengwa kwa Sh.milioni 990.

Alisema daraja lingine lililojengwa ni la Hingiriri lililopo Barabara ya Mwembe/Myamba/Ndungu, ambalo limeigharimu TANROADS Sh. milioni 246.

Kadhalika alitaja Daraja lingine ni la Kikelelwa lililopo Barabara ya Bomang'ombe/Sanya Juu/Kamwanga/Tarakea Polisi katika Wilaya ya Rombo, ambalo limetumia Sh. milioni 436.

Aidha, Kyando, alisema kuwa mvua hizo ziliifanya TANROADS kurejesha huduma ya mawasiliano ya barabara kwa kulijenga upya Daraja la Marangu Mtoni, lililopo Barabara ya Marangu Mtoni/KINAPA, kwa gharama ya Sh. milioni 549.

Daraja hilo liliathiriwa na mvua hizo na kuharibika, licha ya ukweli kwamba lilikuwa finyu na halikuwa na uwezo wa kuruhusu magari mawili kupishana.

Alisema mbali na madaraja hayo pia serikali ilitoa Sh. bilioni 1.722 kwa ajili ya kurejesha mawasiliano na kufanya matengenezo ya miundombinu katika maeneo yaliyoathiriwa na maporomoko ya miamba kwenye Barabara ya Mwembe/ Myamba/ Ndungu, Wilaya ya Same. "Mvua za El-nino, zilisababisha kukatika kwa mawasiliano katika barabara kuu eneo la Hedaru (Same), ambayo ilisomba magogo, mchanga na uchafu sehemu za milimani na kuziba Daraja la Hedaru na kusababisha maji kufurika barabarani.

Vilevile, serikali ilitoa Sh. milioni 160 za kurejesha mawasiliano katika eneo hilo la Hedaru lakini pia ilitoa Sh. bilioni 1.6 kurejesha mawasiliano na kufanya matengenezo maeneo yaliyoathiriwa na maporomoko katika Barabara ya Lembeni/ Kilomeni/ Lomwe." alisema Motta.

TANROADS inahudumia barabara zenye urefu wa kilometa 1,098.83 mkoani Kilimanjaro zikijumuisha kilomita 292.74 za barabara kuu, huku kilomita 806.09 zikiwa ni barabara za mkoa.

Barabara za lami zinazomilikiwa na wakala huyo ni kilomita 518.27 na za changarawe kilomita 580.56.





# Wasimulia namna mikopo asilimia 10 ilivyowakomboa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJASIRIAMALI kutoka Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, walioanzisha viwanda vidogo vya kuongeza thamani mazao ya nafaka kupitia mikopo ya asilimia 10, wameeleza namna mikopo hiyo ilivyowaondoa katika utegemezi.

Walieleza hayo kwa nyakati tofauti kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani na kutaja soko lao kubwa kuwa ni katika shule za msingi, sekondari pamoja na wafanyabiashara wanaopatikana kwenye maeneo yao.

Mwenyekiti wa kikundi cha Mpunze Industry kilichopo Kata ya Mpunze, Therezia Sita alisema mwaka 2022 walipokea mkopo wa Sh.milioni 100 kutoka halmashauri, kati ya hizo Sh.milioni 35 walinunua mashine ya kukoboa na kusaga nafaka, kujenga kiwanda kidogo na kiasi kingine walikitumia kununua nafaka.

Alisema kikundi chao kina wanachama sita na wanazalisha unga wa sembe kuanzia kilo tano, 10 na 25 hali inayowasaidia kujiinua kiuchumi.

Katibu wa kikundi cha Mapinduzi ya Viwanda, Kata ya Uyogo, Hadija Jumanne alisema walikopeshwa Sh.milioni 90, kati ya fedha hizo Sh.milioni 2.4 walinunua kiwanja, Sh.milioni 50 wakajenga kiwanda na Sh.milioni 25 wakanunua nafaka, na sasa wanazalisha mchele na unga kuanzia kilo tano,10, 25 hadi 50.

Alisema masoko yao yanapatikana jijini Dar es salaam, Mwanza, Mkoa wa Tabora na wafanyabiashara wa Mkoa wa Shinyanga kupitia kwa wajasiriamali wenzao.

Mwenyekiti wa Jukwa la Uwezeshaji Wanawake Mkoa wa Shinyanga, Dk. Regina Malimi alisema wamekuwa wakitoa elimu ya biashara kupitia majukwaa ya wanawake yaliyopo kila halmashauri ili kuwawezesha kuwekeza kibiashara kupitia mikopo ya asilimia10, sasa baadhi yao wameanza kunufaika kupitia viwanda vidogo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Ushetu, Morgan Mwita alisema, wamekuwa wakihamasisha jamii kuunda na kusajili vikundi vya wajasiriamali, kuvipatia elimu ya ujasiriamali ili kuviwezesha kujikwamua kiuchumi na kwa sasa wana vikundi vya wanawake 2,006 vilivyosajiliwa.

Alisema katika kuwawezesha wanawake kiuchumi vikundi 52 vimepatiwa mikopo ya Sh.milioni 639.07 isiyokuwa na riba, wameendelea kufanya vema katika nyanja ya kiuchumi kwa kuanzisha ujasiriamali mdogo.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (wa tatu kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wahitimu wa programu ya mafunzo ya uongozi (FFT) kwa mwaka huu, mfanyakazi wa GGML, Kulwa Nyirenda, wakati wa mahafali ya tisa ya mafunzo hayo, yaliyoratibiwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, Makamu Mwenyekiti wa ATE, Imelda Lutebinga (wa tatu kulia), Mwenyekiti Mstaafu wa ATE, Almas Maige (wa pili kulia) na Mkufunzi wa mafunzo hayo, kutoka Chuo cha Mafunzo ya Utawala Afrika Mashariki na Kusini (ESAMI), Prof. Lucky Yona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake GGML wahitimu mafunzo ya uongozi

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wanawake watano kutoka kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) wamehitimu mafunzo ya juu ya uongozi.

Mafunzo hayo yalitolewa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) ambayo ni ya tisa tangu yalipoanzishwa mwaka 2016, hutolewa kwa wanawake ili kuwawezesha kuwa na ujuzi na uwezo wa kushika nafasi za juu za uongozi kwenye kampuni.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana katika mahafali ya tisa ya mafunzo hayo yaliyojumuisha wahitimu 76, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima alizipongeza kampuni zilizowafadhili wafanyakazi wao wanawake.

Alisema serikali itaendelea kuunga mkono programu zinazotekelezwa na ATE hasa ikizingatiwa zinalandana na mipango ya serikali katika kuimairisha na kuhamasisha usawa wa kijinsia.

Waziri Gwajima alisema kaulimbiu ya mahafali hayo yaliyoambatana na mkutano mkuu wa sita wa ATE, inayosema 'Wekeza kwa mwanamke kuongeza kasi ya maendeleo' imekuja wakati mwafaka ambao wizara yake inakwenda kuzindua Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo.

Alisema sera hiyo itazinduliwa Machi 8 mwaka huu ikiwa ni katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Makamu Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayeshughulikia miradi endelevu na masuala ya ubia na ushirika Afrika, Simon Shayo alisema tangu kuanza kwa mafunzo hayo GGML imewezesha wafanyakazi wanawake 23 kupata elimu hiyo.

Alisema baadhi yao wamepandishwa vyeo, huku wawili wakipata nafasi za juu za uongozi ndani ya kampuni hiyo.

Shayo alisema mafunzo hayo yamekuwa chachu kwa kampuni hiyo kwani yameongeza ushirikiano mkubwa kati ya wafanyakazi na kuimarisha usawa wa kijinsia.

Alisema baadhi yao pia wamekuwa na uwezo wa kushindana kimataifa katika nafasi zao ikiwamo wahandisi wanawake.

Mmoja wa wahitimu hao wa GGML, Tammy Sumawe aliushukuru uongozi wa kampuni hiyo kwa kuwahamasisha wanawake kushiriki mafunzo hayo.

Mmoja wa wakufunzi wa mafunzo hayo, Profesa Lucky Yona kutoka Chuo cha Mafunzo ya Utawala Afrika Mashariki na Kusini (ESAMI), alisema wanafunzi hao wamefundishwa namna ya kuongoza, kuzungumza katika mikutano na vikao vya hadhi ya juu pamoja na mafunzo mengine yanayowezesha wahitimu kuwa na sifa za uongozi.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran alisema zaidi ya wanafunzi 400 tayari wamehitimu mafunzo hayo kutoka kampuni mbalimbali nchini.

Alisema mafunzo hayo yamekuwa chachu kwa wanawake kushika nafasi za uongozi na hata katika uandikishaji wa wanafunzi watakaojiunga na mafunzo hayo mwaka huu tayari darasa moja limejaa.

# Mgodi watishia kusitisha uzalishaji kisa uvamizi

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MGODI wa Almasi wa Mwadui Wiliamson Diamond Ltd (WDL) uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu umetishia kusitisha shughuli za uzalishaji kufuatia vitendo vya uvamizi mgodini hapo na ukosefu wa ulinzi imara.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Meneja Uhusiano wa mgodi huo, Benard Mihayo, wakati wa utiaji saini hati ya makubaliano ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia fedha za uwajibikaji kwa jamii (CSR) Sh.bilioni moja na Halmashauri ya Kishapu.

Alisema ombi la mgodi huo kwa serikali wakiwamo viongozi kutoka vijiji 12 vinavyozunguka mgodi huo ni kuwaimarishia ulinzi na kuzuia uvamizi ndani ya mgodi, ili wasisitishe shughuli zao.

Akijibu suala hilo Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, William Jijimya, alisema kupitia vikao vya halmashauri watabuni njia za kuwaimarishia ulinzi pamoja na kutoa elimu kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude alisema mwaka jana walipokea fedha za huduma kwa jamii kutoka kwa kampuni hiyo Sh.bilioni 1.2 ambazo zimetekeleza miradi mbalimbali.

Alisema kwa mwaka huu zimetolewa Sh.bilioni moja ambazo zitaelekezwa kutekeleza miradi ya maendeleo isiyopungua 16, ambapo asilimia 60 ya fedha hizo zinatekeleza miradi ya kimkakati na asilimia 40 zitatekeleza miradi kwenye vijiji 12 ambavyo vinazunguka mgodi huo.

Alisema kwamba watafanya pia marekebisho ya barabara katika stendi hiyo kwa Sh. milioni 32, pamoja na kutengeneza madawati 1,346 ya shule za sekondari na madawati 2,100 kwa shule za msingi kwa Sh.milioni 200.

# Watoto wenye uhitaji Shule ya Mitindo wakumbukwa

**Na Rose Jacob,** MISUNGWI.

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, wanawake mkoani Mwanza wametoa msaada wa mahitaji muhimu kwa watoto wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Mitindo iliyopo wilayani Misungwi.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Mwanza, Jeaneth Shishila alisema hatua hiyo imeratibiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kwa ushirikiano na taasisi mbalimbali za umma na binafsi katika kuhakikisha wanauguza maisha ya watoto hao wenye uhitaji. Alisema miongoni mwa bidhaa walizotoa ni pamoja na mahindi, mchele, mafuta ya kupikia, mafuta ya kupaka, sabuni, dawa za meno, maji ya kunywa, unga pamoja na nguo ikiwa ni sehemu ya kuonesha upendo wa mama kwa mtoto bila kujali aliyonayo.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Hellen Boghohe aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwapa kipaumbele watoto wenye mahitaji maalum nchini kupitia programu mbalimbali.

Boghohe alisema: "Hongereni sana walimu kwa kuwa na mioyo ya upendo hata ukija hapa usiku utakuta watoto ni wasafi, hongereni sana kwa kujitoa kwenu".

# Samia ajiunga nao, pia wanawake vijana kupigania kilimo biashara



Waziri wa Kiimo, Hussein Bashe, katika mradi wa shamba darasa mkoani Dodoma, kwa vijana chini ya dira yake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwalenga vijana na kinamama. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

MUDA mfupi baada ya kukabidhiwa kiti kuongoza nchi, Rais Dk. Samia Suluhu, akaanika kilimo ni sehemu ya mtaji wake kujenga nchi na Watanzania wengi wameajiriwa. Huko ndiko kunakopatikana wenzake, kinamama wengi kazini.

Mwelekeo wake Rais uko katika kilimo cha kisasa na kibiashara, akihimzia bidhaa zake mkulima zifikishwe sokoni, pia kukizalishwa matumizi ya mbolea kisasa, kuwa sehemu kuu iko katika kunakishi tija yake hadi bora shambani.

Huo ndio ukawa mwanzo wa kumea mbolea ruzuku shambani na uzalishaji mbolea viwanda vyake vikimea maradufu.

Leo hii kunasikika misamiati na mageuzi makubwa ya kilimo, ikihamia mazoea ya kilimo cha kisasa na biashara, huku kumezaliwa chombo Mamlaka ya Udhibiti Mbolea, umri wake ukiwa sawa na kipindi Rais Dk. Samia, madarakani.

Simulizi ya bajeti kukua nayo ikashangza umma, ikawa kutoka wastani shilingi bilioni 260 wakati akiingia madarakani, sasa inazungumziwa shilingi trilioni moja.

Vijana wasomi nao wamebuniwa kituo cha kujifunza kilimo cha kibiashara shambani, huko Bahi, Dodoma, mbolea kwa wingi, umwagiliaji na soko kukaribishwa jirani.

Ni aina ya dira inayoitwa BBT kunakokuwapo uwiano wa uzalishaji shamba, soko na miundombinu endelevu, huku makadirio ya mapato na matumizi Wizara Kilimo, ikitangaza makubwa katika kilimo kisasa chenyea mbolea bora, umwagiliaji na miondombinu endelevu kumvusha mkulima shambani.

Ikirejewa mwaka mmoja na nusu wa Dk. Samia kuwa madarakani, Septemba 2022, msimamizi mkuu wake kiserikali Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akatangaza Rais Dk. Samia kuidhinisha shilingi bilioni 150 kutumika kwa ajili ya ruzuku ya mbolea, kuwezesha upatikanaji bidhaa hizo kwa wingi na gharama nafuu.

Hiyo ilikuwa katika msimu wa kilimo 2022/2023, utoaji ruzuku ya mbolea kwa wakulima uliolenga kuongeza uzalishaji chakula, kuwahakikishia Watanzania usalama wa chakula na kukidhi malighafi za viwanda vya ndani.

Ni katika maendeleo zaidi, Agosti mwaka jana, katika kilele cha Maonyesho ya Wakulima, ambako Rais Dk. Samia akamwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kukaa na Wizara ya Fedha kuangalia gharama za usambazaji mbolea ya ruzuku kwa lengo la nafuu wakulima.

Wakiwa katika kilele cha Maonyesho ya Wakulima, Nanenane kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, yakiwa na kaulimbiu ya 'Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula'.

Rais Dk. Samia, akailinda ni kaulimbiu inayotambua mchango wa vijana na wanawake katika kilimo, mifugo na uvuvi.

Akasema katika msimu uliopita walifikisha mbolea hadi ngazi ya kata. Pia, Waziri Mkuu akafafanua mwaka juzi Bungeni kwamba tathmini ya awali ya uzalishaji mazao ya chakula katika msimu wa kilimo mwaka 2021/2022, ambao Rais Dk. Samia alianza kutumikia nafasi hiyo, uzalishaji mazao ya chakula ulifika tani milioni 17.4.

Akasema, kati yake nafaka zilikuwa tani milioni 9.4 na yasiyo nafaka, tani milioni 7.9. Hapo akafafanua: "Mahitaji yote ya chakula yanayojumuisha nafaka na yasiyo ya nafaka kwa mwaka 2022/2023 ni zaidi ya tani milioni 15.

"Tani milioni 9.5 ni za mazao ya nafaka na tani milioni 5.5 ni mazao yasiyo ya nafaka. Kwa kulinganisha uzalishaji na mahitaji, nchi yetu ina kiwango cha utoshelevu wa chakula wa asilimia 115."

Waziri Mkuu akaongeza: "Wastani wa matumizi ya mbolea nchini katika kipindi cha kati ya mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 umeendelea kuwa tani 430,000. Hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2022 upatikanaji wa mbolea nchini umefikia tani 213,403 sawa na asilimia 49.6 ya wastani wa matumizi ya mbolea."

"Yako mambo hayawezi kufanikiwa mara moja, ninyi ni mashahidi Wizara ya Kilimo ni muhimu kwa Watanzania, kwani asilimia kubwa wanaishi vijijini, maisha yao yanategemea kilimo.

# DK. Petronila Ngiloi; mwanamke wa kwanza mpasuaji watoto akidumisha mazito miaka 30

- Kastaafu, Muhimbili wamng'angania; kitaifa wako watano
- Akasimiwa kuumba warithi; ndiye alitenganisha watoto

**Na Christina Mwakangale**



UNAPOTAJA mafanikio ya mtu, taifa na jamii kwa ujumla, upo mchango mkubwa wa wanawake. Wapo walio wanasayansi waliovunja dhana ya kuikimbia tahsusi hiyo.

Daktari Petronilla Ngiloi, Bingwa Mwelekezi Idara ya Upasuaji (Consultant Paediatric Surgeon) Upasuaji Watoto Wadogo akiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ameitumikia taaluma hii zaidi ya nusu ya maisha yake.

Sasa anajivunia mengi, ikiwamo anapotazama watoto aliowatibu wamekuwa, nao wakiwaleta watoto wao na bado anawatibu.

Mmoja wa mashuhuda, yumo katika timu inayowajibikia gazeti Nipashe aliyehangaika na shida ya mtoto wastani miaka mwili, kuanzia umri miaka minne na mitano, hata safari ya kuzunguka kumhangikia ikiwachukua wazazi ziara katika takriban hospitali kubwa nyingi mkoani Dar es Salaam.

Baadaye mzazi akapata ushauri kitaalamu kirafiki kutoka kwa Dk. Vincent Mtweve, wakati huo akiwa Mkuu Kituo cha Kuhifadhi Damu Mtwara, mgonjwa apelekwe kumuona Dk. Petronila Ngiloi, katika Hospitali ya Tumaini, Dar es Salaam, kwamba yu mahiri katika eneo hilo.

Mara moja akiwa mgonjwa wa nje (OPD) tiba ikaanza na tungo tata 'mtoto anasumbuliwa na nini tumboni?' Jibu lake likapatikana ndani ya saa nne pekee, mwenyewe akimfahamisha mzazi 'amehisi kitu fulani kwa uzoefu na ishara ya damu', maana yaliyotarajiwa maabara yamegomkataa.

Mara moja Dk. Ngiloi, akaanza kumpa dozi na ilichukua wiki mbili kuonekana mabadiliko na ndio ukawa mwanzo wa mtoto kupona, huku mzazi akiangukia furaha kubwa.

Cha kushangaza, hata mara nyingine mgonjwa kufika kwake kwa uangalizi, alikuwa na kumbukumbu zake kichwani, ikiwamo maudhui ya faili na tiba. Akadhihirisha 'umama' na taaluma juu!

Haikupita miaka mingi kukashuhudiwa Dk. Ngiloi ambaye sasa ana miaka 69, akiongoza upasuaji wa watoto walioungana, hata umma ukapigwa na butwaa, huku Hospitali ya Rufani Muhimbili, ambako ana mkataba kitaaluma, kukitangaza ushindi wa kihistoria.

Cha kushangaza, hata mteja wake mtoto aliyemtibu katika hospitali ya Tumaini (sasa kidato cha tatu), alipopatiwa gazeti Nipashe lenye picha na habari hizo, aliifurahia, maana alimkariri vilivyo.

Wiki hii gazeti hili katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, imemuangazia bingwa huyo mbobezi wa tiba na upasuaji watoto, akiegemea huko kwa takribani miaka 40.

Hapo Dk. Ngiloi anaanza kudokeza nafasi na majukumu yake makuu kitaaluma akitamka: "...nchini hadi sasa hapa Muhimbili tupo mabingwa wanne tu wanawake, oparesheni kama sio kubwa, naweza kufanya saba mpaka nane, kwa siku kama ni kubwa inaweza kuwa moja au mbili.

"Kwa sababu kuna masuala ya nusu kaputi, pia mtoto aliyefanyiwa upasuaji anaweza kuchukua muda mrefu sana kuamka, hivyo kufanya oparesheni (zingine) zisimame."

Yafuatayo ni mazungumzo yake mstaafu Dk. Ngiloi mwenye taaluma isiyostaafu, akiitumikia Muhimbili hadi leo. Fuatilia:

**SWALI:** Naweza kukufahamu kwa jina nani mtaalamu wa nini, Hapa Hospitali ya Taifa Muhimbili?

**JIBU:** Naitwa Dk. Petronilla Ngiloi ni Mtaalamu Mwelekezi wa Upasuaji wa Watoto Wadogo Muhimbili.

**SWALI:** Taaluma hii uliianza lini, ingawa uanzie katika maisha yako ya tangu mwanzo na kwa nini taaluma hii uliipenda?

**JIBU:** Hii taaluma, upasuaji wa watoto wadogo nina zaidi ya miaka 20. Lakini upasuaji 'general' yaani daktari bingwa wa upasuaji ni kama miaka 30. Nilifanya kwanza upasuaji wa kawaida, halafu nikaamua kujikita kwa watoto wadogo.

**Swali:** Kwa maana kwamba umeitumikia taaluma hii ukifikisha miongo mitano?

**JIBU:** Tangu nimemaliza 'medicine' (masomo ya udaktari ) ni mwaka wa 40 nilimaliza mwaka 1984.

**SWALI:** Kuna sababu ambazo zilikupa ushawishi kusomea fani hii na si nyingine?

**JIBU:** Wakati nikiwa mtoto mdogo, nilikuwa nawapenda sana manesi (wauguzi). Nilikuwa naona wanavyovaa wapo 'smart' (nadhifu) nikapendezwa nao sana.

Nikiwa mdogo shule za msingi nilitamani sana kuwa nesi. Lakini jinsi nilivyoendelea madarasa ya juu, nikaanza kuona kama udaktari ni bora zaidi, kwa sababu anapata fursa ya kuhudumia watu kwa mapana zaidi.

Nilivyokuwa nawaza udaktari, nilikuwa nawaza kwenye suala la upasuaji, lakini vilevile nikawa nimependa sana watoto.

Nikaona kumbe ninaweza nikafanya upasuaji, lakini vilevile nikasema kumbe naweza kufanya kitu ambacho nina- passion nacho, watoto wadogo. Upasuaji wa kawaida yaani 'general study' na baadaye nikaenda kusomea upasuaji wa watoto wadogo.

**SWALI:** je, umesomea wapi (chuo) Katika kuijenga taaluma yako?

**JIBU:** Shahada ya kwanza na ya pili nimesomea hapa hapa wakati Muhimbili ikiwa ni 'Faculty of Medicine' (Kitivo cha Tiba) chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Nilivyokuja kufanya Masters (shahada ya pili) Muhimbili ilikuwa imekwishakuwa ni College of Medicine (MUHAS), na baadaye upasuaji wa watoto wadogo nilikwenda kusomea Afrika Kusini, University of Cape Town, mwaka 2000 hadi 2002.

**SWALI:** Ni kitu gani ambacho umewahi kukifanya katika taaluma yako, unasema kweli hili lilikuwa zito na kitu gani kinakupa ujasiri katika kazi yako?

**JIBU:** Kitu ambacho nimependa sana, na ambacho 'nakiadmire' (anavutiwa) kwa watoto ni wanakuonyesha umri wako katika kazi. Kwa sababu nikiangalia watoto ambao niliwafanyia (upasuaji), sasa hivi ni watu wazima. Na wao wameanza kukuletea na watoto wao, ni kama kichekesho fulani! (aangua kicheko).

Kwa hiyo nikimwangalia huyu nilimfanyia upasuaji akiwa mtoto mchanga kabisa, sasa leo na yeye ameniletea mtoto wake, inaniambia ni kweli nimekuwa katika kazi muda mrefu. Inanipa hamasa, wengine nakutana nao hata siwakumbuki.

'Wamama' wengine nakutana nao, wananiambia ulinifanyia upasuaji mtoto wangu sasa yupo chuo kikuu, sekondari. Ni kitu ambacho kina 'motivate' (kinahamasisha). Watoto wanakuja, wanakuja wakiwa watu wazima nao na watoto wao.

**SWALI:** Je, umewahi kufanya kazi nje na Muhimbili?

**JIBU:** Kwa kuajiriwa hapana. Ila nimewahi kufanya Tumaini kama binafsi. Tulijiunga kikundi cha madaktari, tukaanzisha hospitali binafsi, ingawa hatukufanikiwa sana kama malengo yetu.

Baadaye nikarudi hapa Muhimbili. Tulipata msaada wa wafadhili wakaboresha, wakitoa vifaa kwa ajili ya watoto kuboresha upasuaji wa watoto, vikapatikana vyumba viwili vya watoto.

Nikaitwa kurudi (Muhimbili), nilishastaafu, ili nije kutoa mafunzo kwa kufundisha madaktari na tangu nimerudi mwaka 2017, tuna vijana watano wameshafuzu na wengine wanakaribia kuhitimu.

Wakati mimi nimeingia katika Kitengo kulikuwa hakuna kabisa wataalamu. Alikuwapo Profesa Shija, akiwa daktari bingwa wa Upasuaji watoto wadogo Tanzania, bahati nzuri bado yupo.

Chini yake alikuwapo Profesa Mlay, halafu mimi nilipoingia kulikuwa na madaktari wawili; Dk. Enock Sai, bahati mbaya hawa wametangulia mbele ya haki.

Ikabidi yaanzishwe mafunzo hapa kwetu, kuliko kuwapeleka nje madaktari. Kwanza, inakupa fursa ya kuwaalika madaktari kutoka nje kuja kubadilishana uwezo na kumpeleka daktari nje ni gharama.

SWALIi: Kwa upande wa mwanamke, kuna wengine katika upasuaji?

**JIBU:** Fani ya upasuaji tulikuwa wachache. Kwa hapa Muhimbili upasuaji wa watoto wadogo wataalamu tupo wanne, Bugando yupo mmoja.

Wakati mimi nimemaliza 'general study' (masomi ya jumla) mwaka 1992 nilikuwa mwanamke wa pili Tanzania, wa kwanza alimaliza mwaka 1982. Kwa hiyo utaona tofauti ya miaka 10 kupata mpya, ambaye ndio mimi, nilipatikana mwaka 1992.

Katika utaalamu wa kupasua watoto wadogo, nilikuwa mwanamke peke yangu, sasa ni wanne.

**SWALI:** Unaweza kufanya 'kesi' (idadi ya wagonjwa) ngapi kwa siku katika chumba cha upasuaji?

**JIBU:** Inategemea aina za operesheni, kama sio kubwa zinakuwa saba mpaka nane. Kama ni kubwa, inaweza kuwa moja au mbili.

**SWALI:** Tunaposema mtaalamu upasuaji wa watoto, ni upasuaji wa aina zote yaani mwili mzima? Sio eneo fulani?

**JIBU:** Upasuaji nilipofundishwa ilikuwa unajifunza upasuaji aina zote. Kwa sababu ya ubobezi upasuaji unaohusika umeenda maeneo tofauti. Kwa sasa tunajikita katika upasuaji zaidi wa kifua watoto wachanga ambao mfumo wa chakula haujaungana.

upasuaji wa mfumo wa chakula, kwa sababu wengine wanazaliwa wanashida ya kumeza, saratani, utumbo umejifunga, kushindwa kupata choo, mfumo wa mkojo, jinsi tata.

**SWALI:** Ni kazi gani na mwaka gani ambao uliifanya ukasema kweli hii na inasalia katika kumbukumbu zako?

**JIBU:** Nakumbuka nilivyokuwa Afrika Kusini, nilishiriki kupandikiza ini na kutenganisha watoto walioungana. Ndio upasuaji ambao imenihamasisha na upasuaji unachukua saa nyingi.

Mfano upasuaji wa ini ilichukuwa saa takribani 14 na upasuaji watoto waliokuwa wameungana ilichukuwa kama saa 24. Tulianza asubuhi tukamaliza asubuhi ya kesho yake.

Tulipokezana tu, timu mbalimbali kwa saa kadhaa tofauti. Huyo atakaa saa kadhaa mbili au tatu, hadi zilitimia saa 24.

**SWALI:** Tulikotoka, tangu miaka

**INAENDELEA UK.13**

# Urithi wa Mwinyi kwa Samia ni Fagio la Chuma

**Na Joseph Kulangwa**



TANZANIA kama Taifa, ilianza kuonja uchungu wa mwaka 1972, ilipoondokewa na Makamu wa Rais wake, Shekhe Abeid Amani Karume, aliyeuawa. Watanzania walilia na kuomboleza miaka minane tu baada ya Tanzania kuzaliwa.

Mwaka 1999 ikapata uchungu mwingine, Rais wa kwanza, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, wakalia sana na kuomboleza huku wakishindwa kuamini kama wataishi bila Nyerere.

Wakati Nyerere anafariki dunia, akiwa tayari ameng'atuka madarakani, Karume alikuwa madarakani, wapinga Mapinduzi ya Zanzibar, walipomvizia na kumuua kwa risasi.

Baada ya majonzi ya Rais Nyerere kupungua, mwaka 2000, Watanzania wakampoteza kiongozi mwingine, safari hii akiwa ni Idris Abdul Wakil, aliyekuwa Rais mstaafu wa Zanzibar. Watanzania walilia na kuomboleza.

Ilipofika mwaka 2016, Watanzania wakampoteza Makamu wa Kwanza wa Rais, mstaafu, Aboud Jumbe Mwinyi. Huyu alikuwa Rais wa Pili wa Zanzibar aliyeshika nafasi hiyo baada ya kuuawa Karume. Watanzania kama kawaida, walilia na kuomboleza.

Mwaka 2020 nchi ikaingia tena katika simanzi kubwa, baada ya kumpoteza Rais mwingine mstaafu, Benjamin Mkapa na kufuata mwaka mmoja baadaye, pigo lingine kuondokewa na Rais aliyekuwa madarakani, Dk John Magufuli mwaka 2021.

Hatimaye, Februari 29 mwaka huu, Watanzania wakajikuta tena katika majonzi makubwa na mazito, baada ya kuondokewa na Rais wake wa pili, Alhaji Ali Hassan Mwinyi. Nchi ikazizima tena.

Katika misiba yote hii kama kawaida, Watanzania wamekuwa wakilia, wakiomboleza, wakimsifu marehemu na kuahidi kuwaenzi kwa vitendo kwa mambo mema na mazuri waliyowafanyia.

Siku zinazotolewa kuomboleza, hujibainisha kwa bendera kupepea nusu mlingoti, wanasiasa kufunguka walivyowajua marehemu na kuwa karibu nao, walivyosikiliza na kupokea ushauri wao na mambo mengi ya kuvutia.

Ni wakati vyombo vya habari hujikuta vinaelezea mema ya viongozi hao, walichokifanya wakati wa uhai wao na michango yao kwa jamii hususan yenye tija kwa Watanzania.

Muda huo, viongozi wa kitaifa hujitokeza wakajiapiza kufuata nyao za waliowatangulia, hasa katika mapambano ya kulinda mali na rasilimali za Taifa, pia kuwaletea wananchi maendeleo na kusimamia amani, utulivu na mshikamano.

Ni wakati wananchi hujitokeza kujisahaulisha mabaya waliyofanya wakati wakiongozwa na hao waliotangulia mbele za haki, siku ya maombolezo wakijinasibu waliwapenda na kuwasaidia kiuongozi.

Hata hivyo, giza katika nuru halijifichi, watu hao hujulikana, lakini huachwa waendele na yao, huku wananchi wakiheshimu uamuzi wa Muumba na kuwahifadhi ndugu zao kwa maisha ya peponi.

Jambo la msingi kwa viongozi wanaotoa ahadi za kuwaenzi watangulizi, ni kuhakikisha wanafanya hivyo kwa maslahi mapana ya wanaowaongoza, kuliko kwenda kinyume cha matarajio ya wanaoongozwa.

Ni kawaida kuwa kila kiongozi anapoingia madarakani, kuahidi kupambana na maovu dhidi ya wananchi, ukiwamo ubadhirifu wa mali za umma na mengine yanayokwaza maendeleo ya wananchi. Pia, kulinda wanyonge dhidi ya wenye nguvu.

Mwalimu Nyerere, alikemea uonevu katika jamii, pia unyonge. Alikataa unyanyasaji, pia akataka kuona umasikini miongoni mwa wananchi unatoweka, ujinga na maradhi vinakoma.

Yote hayo aliyafanya kwa kutarajia wasaidizi wake wanamsaidia, hata kama hayupo madarakani au duniani, basi mapambano hayo yanaendelezwa na waliomfuata.

Alhaji Mwinyi alipoingia madarakani katika mazingira magumu ya kiuchumi, aliahidi kukabiliana na hali hiyo, akimrithi mtangulizi wake.

Alifanya hivyo kwa nguvu zake na hakika alifanikiwa kufanya Watanzania wasahau walikotoka. Ukaingia wakati, baadhi ya watendaji wakitumia fursa za matatizo ya wananchi kujitajirisha.

Mzee Mwinyi akaja na 'Operesheni Fagio la Chuma' kupambana na wabadhirifu wa mali za umma. Hata hivyo, fagio liliota kutu na kukaa stoo.

Kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, ndiye mwenye hatamu za uongozi hivi sasa na amemwelezea vizuri sana marehemu Mwinyi jinsi alivyoliongoza Taifa kwa mwelekeo mzuri, ni dhahiri naye atapita njia hiyo hiyo kusaidia Watanzania.

Rais Samia amezungukwa na watendaji baadhi wasiotenda vema, hivyo anapaswa kwenda nyumbani kwa Mwinyi angalau akarithi lile fagio, na kama liko stoo alichukue alisafishe, aanze kufagia hawa wanaotaka kumkwamisha.

Tunaona tunavyopita kwenye taka iwe umeme, maji, na sukari. Fagio hilo litumike kwenye marundo ya taka na kuyasafisha, ili wananchi wapite humo hata bila kuvaa viatu.

Roho za marehemu hawa ziendelee kulazwa pema peponi. Amina.

## DK. Petronila Ngiloi; mwanamke wa kwanza mpasuaji watoto akidumisha mazito miaka 30

**INATOKA UK.12**

hiyo unaonaje kukua kwa huduma za afya nchini, ikilinganishwa na miaka hii?

**JIBU:** Tulikotoka, tulipo sasa ni tofauti. Mfano 'canulla' (cannula, is a small plastic tube, is inserted into one of the veins in your arm using a needle.), nilienda kuiona Afrika Kusini kwa mara ya kwanza, hatukuwa nazo.

Zamani ilikuwa ukimuwekea mtoto dripu, unamwambia mama ilinde kama mboni yako, kwa sababu tulikuwa tunatumia sindano. Ikicheza tu kidogo, inahama kwenye mshipa. Watoto walikuwa wanakuja wana shida nyingi. Ukiwa zamu usiku hulali kwa sababu ya kulinda dripu.

Kazi kubwa ilikuwa kuweka 'lani' za watoto wadogo na ndio maana kuna wakati madaktari wakaenda wengi kusomea eneo hilo tu ikawa kama fani. Vifaa vya upasuaji pia vilikuwa vichache, mfano hizi glovu baada ya upasuaji zilikuwa zinachukuliwa zinafuliwa, zinaandaliwa baadaye zinarudiwa tena kuvaa.

Kuna kipindi ambacho hata dawa ikiisha muda wake, kama antibaiotiki kulikuwa na ruhusa maalum ya miezi sita kutumia baada ya 'expire date' (siu ya ukomo), kuliko kukosa kabisa bora uwe nayo hiyo dawa. Hata sindano za kuchoma wagonjwa zilirudiwa tena, zilikuwa zinachemshwa zinatumika.

Kuna vitu ambavyo vimeondoka kabisa, hata ukisimulia sasa mtu hawezi kudhania, imebaki historia. Ila watu walikuwa wanapona, tuliona ni kawaida. Kwa sasa vifaa vya kisasa imefanya maisha yamekuwa rahisi sana.

Mfano kama 'CT Scan' na MRI, hazikuwapo. Tulitumia historia zaidi ukielezewa, mikono kupapasa, akikusimulia basi unahusianisha tu na ukienda ukifungua tumbo, unakuta kweli ulichokuwa unakifikiria. 'Ultra sound' hazikuwapo, 'Scanner' pekee ilikuwa ni 'X ray' tu, ambayo ilitusaidia kuthibitisha ugonjwa. Lakini sasa, kuna vifaa ambavyo vinagundua kitu kidogo au ambacho kingewza kugundulika miaka minne au mitano baadae, inakuonyesha sasa mapema, hata saratani.

**SWALI:** Watoto wamegawanyika katika makundi matatu; watoto wachanga; watoto chini ya miaka mitano; watoto chini ya miaka 18. Je, wewe unashughulikia zaidi kundi lipi?

**JIBU:** Ni watoto wachanga, tangu kuzaliwa hadi miaka 12.

**SWALI**: Shida kuu ya watoto wengi unaowahudumia ni nini?

JIBU: Mara nyingi ni hitilafu za tangu kuzaliwa ambazo zinarekebishwa.

**SWALI:** Je, una mrithi wa fani yako? Yaani kuna watoto wako, au mmoja anatamani kuwa kama wewe?

**JIBU:** ...(kicheko), Hapana! Ila kuna mmoja angalau naweza kusema ndio, ni Mfamasia. Nina watoto wanne, mfamasia huyu ni msichana.

# Mwendesha bodaboda aliyeanza vita maisha akiwa 'hausigeli' Dar

- Leo yuko darasani, anamiliki pikipiki yake
- Asimulia anavyopangua 'i love you' kazini

**Na Sabato Kasika**

MOJA ya mambo ambayo wanawake wamekuwa wakikazania, ni usawa wa kijinsia lengo likiwa kuongeza uwakilishi ili idadi yao iwe 'asilimia 50 kwa 50', kati yao na wanaume, katika vyombo vya maamuzi.

Pia, kazi ambazo zamani zilichukuliwa kama za wanaume, kama udereva wa pikipiki, bajaji, magari madogo na makubwa, yakiwamo mabasi na malori, sasa nao wameamua kujitosa huko.

Ingawa idadi yao hailingani kama ya wanaume, lakini wapo ambao wanafanya kazi hiyo katika maeneo mbalimbali ikiwamo jijini Dar es Salaam ambako wapo sasa madereva wa bodaboda.

Wakati leo ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Nipashe imezungumza na mmoja wa madereva hao wa bodaboda, Veronica Mgaya maarufu 'Mama Love', ambaye kijiwe chake cha kazi kipo Kimara Baruti.

Nipashe inafika katika kitongoji hicho kumuulizia na kuelezwa kuwa hayupo, lakini baadhi ya madereva wenzake wa kiume wanaanza kuelezea sifa zake na jinsi wanavyoshirikiana naye.

"Mama Love atakuwa amepeleka abiria, kwani wengi wanamkimbilia kuliko sisi, anawazidi baadhi ya vijana wa kiume. Ni jasiri katika kazi hiyo ambayo ni mara chache kukuta mwanamke anaifanya," anasema mmoja wa madereva ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini.

Baada ya kusikia sifa hizo, Nipashe iliamua kupiga kambi eneo hilo kumsubiri Mama Love, ikiwa inawasiliana naye kwa simu, lakini akasema yupo darasani, hivyo hawezi kuwahi kurudi.

Kutokana na maelezo hayo, Nipashe iliondoka kwa ahadi ya kuonana kesho yake (juzi) kwa ajili ya kufanya naye mazungumzo, kujua mengi ya yanayomhusu katika kazi hiyo, ambayo ina madereva wachache wanawake.

Baada ya kushuhudia sifa nyingi ambazo madereva wenzake wanamwagia Nipashe, ikatamani kujua kwa kina kuhusu historia ya maisha yake na jinsi alivyoingia kazini, hata ikafikia ahadi ya kukutana naye .

**SWALI:** Unawezaje kuelezea historia ya maisha yako kwa kifupi?

**JIBU:** Sawa, mimi nilizaliwa wilaya ya Kilolo mkoani Iringa miaka 36 iliyopita nikiwa mtoto wa kwanza katika familia yetu ya watoto nane. Ninaishi pekee yangu, nina mtoto mmoja wa kike mwenye umri wa miaka 13.



Veronica Mgaya akiwa na waendesha bodaboda wenzake, Kimara Baruti, Dar es Salaam.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

Baada ya kumaliza elimu ya msingi mwaka 2006, nilikuja jijini Dar es Salaam kutafuta maisha kwa kufanya kazi za ndani hadi mwaka 2016.

Nilipoacha na kuingia katika udereva wa bodaboda kwa kufundishwa na vijana madereva wa mtaani kwetu huku Baruti (Kimara).

Baada ya hapo nikapata pikipiki na kuanza kuingia barabarani kufanya kazi hadi leo ninaendelea na kazi hii ya kusafirisha abiria huku na kule katika jiji hili la Dar es Salaam.

Nimeingia katika hii kazi bila kushawishiwa na mtu, bali kwa kutambua kwamba hakuna kazi ya mwanaume.

**SWALI:** Tangu uanze kazi ni changamoto gani unakumbana nazo?

**JIBU:** Kwanza kabisa, ilikuwa si rahisi kupata abiria, badala yake walikuwa wananishangaa. Ninadhani mimi ni miongoni mwa watu wa mwanzo kabisa (wanawake) kuendesha bodaboda, hivyo watu walikuwa hawaamini kwamba mwanamke anaweza kufanya kazi hii.

Lakini, kadri miaka inavyokwenda, tayari wamezoea na sasa wengi wamekuwa wakinikimbilia kupata usafiri, wanasema dereva mwanamke yuko makini kuliko vijana wa kiume.

Siwezi kuwabishia, kwa sababu wao ndivyo wanavyoniona nikiwa barabarani. Lakini hata hivyo, mwenyewe ninajiamini. Huu ni mwaka wa nane niko barabarani, sijawahi kupata ajali yoyote kubwa zaidi ya rabsha za kawaida barabarani.

Ninajua kwamba ajali haina kinga, lakini zipo ajali nyingine za kujitakia. Wakati mwingine unakuta dereva wa bodaboda anashindana na magari makubwa eti anataka kuyapita.

Mtindo huo ni miongoni mwa visababishi vya ajali nyingi za bodaboda. Aidha, enzi hizo ninaanza kuingia barabarani, kulikuwa na wimbi la uporaji wa pikipiki, ila Mungu alinijalia sikuwa nikikutana nalo.

Uporaji huo ulinitia hofu, lakini nilikomaa hadi sasa ninaendelea na kazi. Pamoja na hayo, kuna changamoto nyingine ambayo ninakumbana nayo kutoka kwa abiria wa kiume, baadhi yao wanaomba namba yangu ya simu kwa maelezo kwamba wakitaka usafiri wanipigie, kumbe lengo lao ni kutafuta uhusiano kwangu.

Binafsi ninakerwa na tabia hiyo. Si vyema kuingiza uhusiano kwenye biashara. Nitawakubalia wangapi? Wito wangu ni kwamba, wasinichukulie kama ninatafuta mabwana, mie niko kazini kama wanavyofanya wengine, sikuja barabarani kutafuta wanaume.

Vilevile niwashauri wanawake wenzangu ambao wanajiuza au kusimama barabarani kuomba fedha kwa madereva abiria wa mabasi. Kazi za kufanya zipo nyingi kuanzia biashara ndogondogo na hata udereva wa bobaboda au bajaji. Tusingojee kuomba, kujiuza au kuletewa.

**SWALI:** Pikipiki unayoendesha ni yako, au ina mwenyewe?

**JIBU:** Wakati ninaanza kazi, nilikuwa ninatumia pikipiki ya tajiri yangu, lakini baadaye nilipata ya kwangu baada ya kuingia mkataba na bosi mmoja kufanya kazi kwa mmoja ili ukiisha pikipiki inakuwa yangu, kwa hiyo ninamiliki pikipiki yangu tangu mwaka 2018.

Ninaitunza sana na niko makini kuhakikisha chombo changu kinaendelea kuwa kizima kwa sababu ndicho kinachonipa rikizi na kumlipia mwanangu ada ya shule hata ada yangu mwenyewe, kwani kwa sasa ninasoma katika kituo kimoja hapa Dar es Salaam ili nipate elimu ya sekondari, kwani kama nilivyokueleza awali, nilihitimu elimu ya msingi na kuja kufanya kazi za ndani ambazo nimeshaachana nazo na kuwa dereva wa bodaboda.

Ila kile ninachopata kila siku katika kazi hii ni siri yangu, si vizuri kutangaza nisije kuonekana kwa baadhi ya madereva wenzangu kuwa ninajisifu.

Jambo la kuzingatia wakati huu wa maadhimisho ya siku ya wanawake ni kwamba wanawake wasihofie kufanya kazi kama hii au nyingine ambazo awali zilichukuliwa kama za wanaume.

**SWALI:** Nini malengo yako ya baadaye katika kazi hii?

**JIBU:** Ninatamani kuwa dereva wa magari makubwa yakiwamo malori yanayosafirisha mizigo ndani na nje ya nchi, hivyo, hilo ndilo lengo langu, pia ninatamani kupata elimu ya sekondari ambayo tayari nimeanza masomo ili hata nikifikia kuwa dereva wa magari makubwa, niwe tayari nina uelewa wa kutosha wa lugha ya kigeni ili iwe rahisi kuwasiliana na madereva wengine wa nje ya nchi.

Ninataka niwe miongoni mwa madereva wanawake wa Tanzania ambao tumekuwa tukiwashuhudia wakihojiwa kwenye vyombo vya habari, kwa hiyo hii kazi ya udereva wa bodaboda ni mwanzo wa kujiandaa kuwa dereva wa magari makubwa.

Ninaamini ninaweza kwani penye nia pana njia. Ipo siku lengo langu hilo litatimia. Ninawatia moyo wanawake wenzangu ambao wapo nyumbani, watafute ajira za kuendesha bodaboda, kwani kazi hii si ya wanaume tu.

**SWALI:** Ujumbe wako kwa wanawake wenzako ni upi?

**JIBU:** Ujumbe wangu ni kwamba dunia imebadilika na inakwenda kasi sana, hivyo si wakati wa mwanamke kubaki nyuma na kuanza kulalamika, wachangamkie kila fursa halali inayopatikana, si kusubiri kusukumwa kufanya kazi, bali mwenye nia ya kuendesha bodaboda, kuuza genge, kushona nguo na shughuli nyingine afanye sio wakati wa kusubiri kuletewa mahitaji nyumbani.

Wote tumeumbwa tukiwa na uwezo sawa, tofauti ni maumbile tu, ambayo hayawezi kutufanya tujione kama hatuna nguvu za kufanya kazi.



# ‘Wapelekeni shule watoto wa kike wawe viongozi baadaye’

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

SERIKALI imewataka wazazi wilayani Mkalama mkoani Singida kuacha tabia ya kuwaficha na kuwaozesha watoto wa kike, badala yake wawapeleke shule ili wawe viongozi wa baadae watakaolitumikia taifa kwa uzalendo mkubwa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos aliyasema hayo jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kiwilaya katika Kata ya Ntumuli wilayani hapa.

Messos ambaye alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali katika maadhimisho hayo, alisema watoto wa kike wakipelekwa shule wanategemewa kuja kuwa madiwani, wakurugenzi, wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa na madaktari bingwa wa kutibu wanawake.

Alisema tatizo la ukatili wa kijinsia limeendelea kuwepo katika Wilaya ya Mkalama na Mkoa wa Singida, hivyo ni jukumu la wanawake kuhakikisha wanalea watoto na vijana katika maadili yaliyomema ya kumpendeza Mungu, yenye mlengo wa kuwa waadilifu na wazalendo kwa taifa.

“Kijana wangu akimheshimu kijana wako ukatili utapungua kwa asilimia kubwa, kwa hiyo pamoja na mihangaiko ya kazi wanawake tujitahidi katika jukumu letu la msingi la kulea watoto wetu vizuri ili wawe mabalozi wazuri wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia,” alisema. Mkurugenzi huyo alisema watoto wakiachwa kuwa na maadili mabaya mwisho wa siku vitendo ukatili wa kijinsia wanawafanyia mama zao au wazazi wao kutokana na wanawake kutotumiza jukumu lao la msingi la kuwaleta katika maadili mema.

Messos alisema serikali imeendelea kuboresha maendeleo katika Wilaya ya Mkalama kwa kuleta fedha za kujenga miradi mbalimbali katika sekta za afya, elimu na miundombinu ili kuwawezesha wananchi kupata huduma bora.

Alitoa mfano hivi karibuni Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ilipokea Sh.milioni 600 kwa ajili ya kununua vifaa tiba katika vituo viwili vya afya ambavyo ni Bomanga na Irunda na Sh.milioni 150 zimeletwa kwa ajili kununua vifaa tiba katika zahanati zote mpya zilizoanza kutoa huduma katika wilaya hiyo.

“Niwapongeze wananchi wa Tumuli kwa kuanzisha ujenzi wa boma la zahanati, sisi kama halmashauri kwa kutambua umuhimu wa zahanati hiyo tutahakikisha tunaliombea bajeti maalum ili lijengwe na kukamilika ili wananchi waanze kupata huduma za matibabu,” alisema.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kugombea katika nafasi mbalimbali za uongozi ili kushiriki katika maamuzi mbalimbali ya maendeleo.



Wakili Mkuu wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Chivanenda Luwingo (mwenye miwani), pamoja na wafanyakazi wenzake wakikabidhi msaada wa vitu mbalimbali zikiwemo sabuni na mafuta kwa mgonjwa Salma Hussein aliyelazwa kwenye Hospitali ya Rufani ya mkoa wa Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. PICHA: PAUL MABEJA

# Bil.10/- kuimarisha upatikanaji haki wanawake

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Legal Services Facility (LSF) na Enabel, Shirika la Maendeleo la Ubelgiji wametia saini mkataba wa ruzuku ya Sh. bilioni 10.7 kwa lengo la kuimarisha huduma ya upatikanaji wa haki kwa wanawake kupitia msaada wa kisheria.

Mradi huo shirikishi unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) chini ya mradi uitwao “Gender Transformative Action: Breaking the Glass Ceiling” lengo lake ni kupunguza unyanyasaji wa kijinsia na kuongeza usawa katika upatikanaji wa haki hususani kwa wanawake na wasichana.

Wakati wa utiaji saini wa mkataba huo, Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng’wanakilala, alisema kupitia mradi huo, LSF itahakikisha kuwa huduma za msaada wa kisheria zenye ubora zinapatikana kwa watu wote kupitia mifumo rasmi na isiyo rasmi ya utoaji haki.

Lulu alisema mradi huo utaongeza uelewa wa jamii hususani wanawake na wasichana kuhusiana na umuhimu wa msaada wa kisheria.

“Tuna furaha kutia saini mkataba huu na Enabel kwa kuwa umelenga katika kufikia malengo na hatua zote muhimu katika kuboresha upatikanaji wa haki kupitia huduma za msaada wa kisheria hasa kwa wanawake, wasichana, na jamii zote. utatekeleza Tanzania nzima,” alisema.

Mwakilishi Mkazi wa Enabel nchini, Koenrad Goekint, alisema ushirikiano huo ni wenye nia ya kuimarisha upatikanaji wa haki, hasa kwa wanawake, wasichana na jamii zilizotengwa.

Alisema: “Ushirikiano huu unathibitisha dhamira yetu ya kukuza maendeleo endelevu na kujenga jamii iliyo na usawa katika upatakanaji wa haki na inayoshiriki kikamilifu katika mfumo wa sheria”.

Balozi wa EU Afrika Mashariki, Christine Grau, alisema kupitia mradi huo EU inaendelea kushirikiana na wadau katika kuongeza upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana hasa wale ambao ni waathirika wa ukatili wa unyanyasaji wa kijinsia.

Grau alisema: “Kwa hakika mradi huu unakwenda sambamba na juhudi zingine zenye nia ya kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuongeza ushiriki wao katika uongozi na uwakilishi wao katika vyombo vya

# Wagonjwa waliolazwa muda mrefu hospitali wakumbukwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Mashtaka (NPS) imetoa fedha kwa ajili ya matibabu kwa wagonjwa waliolazwa kwa muda mrefu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Wakili wa Serikali Mkuu kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Chivanenda Luwingo, alibainisha hayo jana jijini hapa baada ya kukabidhi msaada huo kwa wagonjwa na uongozi wa hospitali hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika viwanja vya hospitali hiyo alisema msada huo ni sehemu ya matendo ya huruma wakati huu wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

“Kuelekea siku hii sisi wanawake wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka tulikuja hapa kuona changamoto zilizopo kwa wagonjwa, hivyo tukabaini uwepo wa wagonjwa wa muda mrefu ambao gharama za matibu kwao zimekuwa kubwa na wameshindwa kuzimudu.

“Hivyo leo hii tutawalipia gharama za matibabu wagonjwa hawa wa muda mrefu watano ambapo wanawake ni wawili na wanaume watatu pamoja na mtoto mmoja ambaye anahitaji gharama za upasuaji na dawa kwa muda wa siku saba, gharama za matibabu yote ni Sh. 900,000”alisema.

Alisema pamoja kugharamia matibabu hayo pia wametoa vitu mbalimbali kwa manusura wa ukatili wa kijinsia ikiwemo watoto waliotelekezwa na wazazi wao.

“Tumetoa msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto manusura wa ukatili ambao waliputwa na wazazi wao, hivyo wanahitaji vitu kama nepi, maziwa pamoja na dawa mbalimbali. Lakini pia tumetoa msaada wa sabuni na mafuta kwa wagonjwa wa kawaida, gharama zote ni Sh. milioni mbili” alisema.

Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaani Mkoa wa Dodoma, Stanley Mahundo, aliishukuru Ofisi ya Taifa ya Mashtak kwa msaada huo ambao utakwenda kusaidia wagonjwa wenye uhitaji.

“Tunaishukuru sana Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa msaada huu na tunaahidi kuwa tutahakikisha msaada huu unawafikia walengwa na nitoe wito kwa watu wengine kujitoa kusaidia wagonjwa kama hawa wenye uhitaji “alisema.





# Polisi yapewa msaada kuimarisha doria, usalama barabarani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limekabidhiwa magari mawili na pikipiki mbili kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu hasa operesheni, kuimarisha usalama barabarani na doria.

Vyombo hivyo vimekabidhiwa kwa jeshi hilo na Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake kwa jeshi hilo, hasa kupunguza matukio yanayohusu usalama barabarani.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya Jeshi la Polisi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishina Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga aliishukuru kamati kwa msaada huo akieleza kuwa utasaidia kupunguza tatizo la upungufu wa vifaa.

Alisema jeshi hilo limekuwa likifanya operesheni na doria kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo kwa ajili ya kuimarisha usalama lakini kikwazo kikubwa imekuwa ni uhaba wa vifaa.

"Kwanza nawashukuru sana wadau wetu kwa msaada huu, tunaamini kwamba magari haya pamoja na pikipiki yatatusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa vifaa hivi, tunaamini kwamba ufanisi wetu katika kutekeleza majukumu yetu utaimarika," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema magari hayo yatatumika kufanya doria kwenye barabara kuu zinazopita katika mkoa huo kuelekea nchi jirani na mikoa jirani ikiwemo Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) na Barabara ya Mbeya Kyela.

Akikabidhi vifaa hivyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, mhandisi Rajabu Ghuliku alisema vifaa hivyo ni sehemu ya majukumu ya kamati hiyo katika kulisaidia Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu yake.

"Kamati imeona ni vema kutoa msaada wa pikipiki na magari kwa jeshi letu la polisi Mkoa wa Mbeya ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu hasa kwenye eneo la usalama barabarani," alisema Ghuriku.

Hivyo, aliwaomba wadau wengine kulisaidia jeshi hilo kupata vifaa mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

# Wauza samaki, maofisa serikali waingia katika mgogoro

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO umeibuka baina ya wajasiriamali wanaouza samaki katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya na maofisa wa serikali waliokuwa wanaendesha operesheni ya kuwakamata wajasiriamali hao, kwa madai ya kufanya biashara hiyo bila kuwa na vibali.

Maofisa hao wanaodaiwa kutoka katika Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kitengo cha kilimo, mifugo na uvuvi wanadaiwa kuvamia maeneo ya wajasiliamali hao usiku, kupora samaki na kuzifungia ofsini hali ambayo inawasababishia hasara.

Juzi wajasiriamali hao waliiomba serikali kuwasaidia kuwaondoa maofisa hao wakidai kuwa operesheni wanazozifanya siyo halali kutokana na maofisa hao kuingia mitaani na kuanza kuwakamata muda ambao siyo wa kazi na kwamba hawana elimu yoyote kuhusiana na vibali vinavyotakiwa.

Happy Mwaipungu alisema maofisa hao walipohifadhi samaki zao ofsini waliwataka kulipa Sh. 20,000 ili wawarejeshee bidhaa hizo, huku pia wakilazimishwa kujiunga kwenye chama cha wafanyabiashara wa samaki kwa gharama ya Sh. 200,000.

Alisema mtaji wake ni Sh. 5,000 na hivyo hana uwezo wa kulipa gharama zinazohitajika na hivyo akaiomba serikali iwasaidie ili waweze kufanya biashara yao kwa uhuru.

"Sisi hapa asilimia kubwa mitaji yetu ni chini ya Sh. 10,000 kwahiyo hatuna uwezo wa kulipa Sh. 20,000, tunapata faida kidogo sana kwenye biashara hii kwa ajili ya kutusaidia kuendesha maisha na watoto wetu," alisema Happy.

Esther Jackson alisema maofisa hao baada ya kuwapora samaki zao hawakuhifadhi kwenye ofisi ya serikali na badala yake wakahifadhi kwenye ofisi ya chama cha wafanyabiashara wa samaki wanaouzia ndani ya Soko la Tarafani.

Alisema wao wanauza nje ya soko ambako wanalipa ushuru na mapato mengine ya serikali na kwamba hawauzi muda wote na badala yake wanauza kuanzia jioni muda ambao walikubaliana na wafanyabiashara wa ndani ya soko ili kutoingiliana.

Alisema baadhi ya samaki waliochukuliwa walikuwa wamehifadhiwa kwenye ndoo hali ambayo itasababisha samaki hao kuharibika na kuwaingiza hasara.

"Samaki wakikaa muda mrefu kwenye vindoo wanaharibika kwahiyo tunaiomba serikali itusaidie maana gharama wanazotaja sisi hatuwezi kulipa na tunadhani samaki wetu watakaharibika," alisema Esther.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wadogo maarufu kwa jina la machinga Kata ya Utengule Usongwe, Calvin Lunda alisema baada ya maofisa hao kukamata bidhaa za wajasiriamali waliamua kuwahoji lakini hawakuwapa ushirikiano.

Alisema waliamua kuwasiliana na Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda ambaye alisema hajawatuma wakafanye kazi hiyo jambo ambalo liliwapa wasiwasi.

Alisema muda ambao maofisa hao waliingia ulikuwa ni muda ambao sio wa kazi kwa maofisa wa serikali na hivyo wakahisi kwamba pengine walikuwa ni wahuni.

Gideon ambaye ni Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alikiri kutokea kwa mgogoro huo na kwamba kilichosababisha ni wajasiriamali hao kutokuwa na uelewa wa taratibu za kuuza samaki.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya uvuvi, mtu yeyote anayefanya biashara ya mazao ya uvuvi ni lazima awe na vibali na kwamba Sh. 20,000 ambazo wajasiriamali hao walikuwa wanatozwa ni kwa ajili ya kuwakatia leseni.

Alisema leseni za biashara ya mazao ya samaki zinatofautiana kulingana na ukubwa wa biashara kwa maelezo kuwa bei hizo zinaanzia Sh. 20,000 na kuendelea.




Mkuu Msaidizi wa Gereza la Ruanda upande wa Wanawake, ASP Enea Mwaisemba (wa tatu kulia), akipokea msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo taulo za kike, kutoka kwa wajumbe wa Taasisi ya Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO) na Twende Wote Foundation, kwa ajili ya wafungwa wanawake, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, jijini Mbeya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi kada ya afya wapewa angalizo ujazaji PF3

**Na Elizabeth John,** MAKETE.

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe limewataka watumishi kada ya afya kuzingatia ujazwaji wa fomu namba tatu (PF3) na kuepuka udanganyifu, ili kusaidia taifa katika mapambano dhidi ya kesi za ubakaji.

Wito huo ulitolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga wakati akizungumza na watumishi wa Hospitali ya Consolatha Ikonda wilayani Makete.

Kamanda Banga alisema ni vizuri wakawa wawazi katika kuzaja fomu hizo hasa kwenye matukio ya ubakaji.

"Anapoletwa mtoto mdogo kafanyiwa kitendo ha ubakaji na daktari umeona kabisa katika tukio hilo kuna viashiria vya mananii basi tunaomba mfanye vipimo ili kupata zile mananii ili baadaye twende tukazilinganishe na mananii za yule mtu ambaye tumemtuhumu ili mwisho wa siku tupate muunganiko," alisema Kamanda Banga.

Kamanda Banga alisema kuwa watumishi wengi wakishaona wanasema wameona mchubuko kwamba tayari mtu huyo kaingiliwa. "Tunaomba twende mbali zaidi ili tuweze kupata mafanikio, mahakamani bila sayansi haiwezekani, itakuwa ni ngumu sana kuthibitisha baadaye na matokeo yake wahalifu wanaendelea kupita mitaani kwamba sheria haiwezi kuwachukulia mkondo," alisema Kamanda Banga.

Baadhi ya wakazi wilayani Makete akiwemo, Getruda Ngimbuchi na Alex Sanga walisema ni kweli kesi nyingi zinaishia kwa watuhumiwa kuachiwa, hivyo inawezekana kuwapo kwa udanganyifu katika fomu namba tatu.

Wapo watu tunawaona kweli walifanya ubakaji kwa watoto lakini wanaachiwa hii inawezekana kwa sababu labda ya rushwa kwa aliyetenda kosa hilo kwenda kwa daktari na kuongea nae ajaze tofauti ili aachiwe," alisema Ngimbuchi.

Sanga aliwataka madaktari kuzingatia weredi katika kazi yao ili kusaidia jamii kwenye matukio ya ubakaji kwa kutenda haki.

# Wanawake wajasiriamali walivyoaga umaskini

## -Mwani sehemu ya mtaji, watengeneza ajira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI leo dunia ikiadhimisha Siku ya Wanawake, lakini kundi hilo bado ni waathirika wakubwa wanaokabiliwa na hali ngumu ya maisha, wengi wao wanatafuta njia mbadala ya kujikwamua.

Wengi wao wanatumia njia ya ujasiriamali ambayo inaonekana kuwa ni mkombozi kwao, kwamba wengi wamepata mafanikio kutokana na kuondokana na utegemezi kutoka kwa wanaume kwa asilimia 100.

Visiwani Zanzibar zaidi ya asilimia 60 ya wanawake wenye uwezo wa kufanya kazi wamejiajiri katika ujasiriamali wa aina tofauti ikiwemo biashara ndogo ndogo na uzalishaji wa bidhaa kwa kutumia malighafi za ndani na nje ya nchi.

Nafasi ya mwanamke kujikomboa kiuchumi imezidi kupata nguvu kutokana na baadhi ya wanawake kuonesha mafanikio makubwa katika kazi za ujasiriamali ambazo kwa kiasi kikubwa imekuwa ni fursa za ajira kwa wanawake wengi hapa Zanzibar.

Mmoja wa wanawame hao shupavu ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Tanzania (TWCC) tawi la Zanzibar, Tatu Suleiman (41).

Tatu ambaye pia ni Mkurugenzi wa kiwanda cha Zaidat kinachotengeneza vipodozi vya asili vinavyotokana na mwani na spaice ikiwemo karafuu katika mahojiano yake na Nipashe anasema alianza biashara hiyo akiwa na mtaji wa Sh. 50,000 mwaka 2012.

Anasema wakati huo alikuwa peke yake lakini kwa sasa anaingiza faida kubwa na amefanikiwa kuwaajiri vijana nane wa jinsia tofauti, kwamba kiwanda chake kipo Mtaa wa Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar.

Tatu anabainisha kwamba alipata wazo la kufanya biashara hiyo kutokana na hali ngumu ya maisha na kiuchumi na ndipo alipohamasika baada ya kushiriki makongamano mbalimbali ya wanawake na kuanza kujifunza masuala ya ujasiriamali.

"Mwanzo nilipata mafunzo ya utafiti wa mimea na ndipo nikaanza kutengeneza bidhaa za vipodozi vitokanavyo na mimea na nashukuru bidhaa nilizotengeneza nilipopeleka katika taasisi za viwango na vipimo ikapitishwa bila ya matatizo yoyote" anasema.

Anabainisha kuwa kwa sasa amejikita zaidi katika kutengeneza vipodozi baada ya kuona wanawake wengi wanatumia vipodozi vyenye kemikali na huwaathiri ngozi zao, hivyo akalazimika kutengeneza vipodozi visivyo na kemikali na soko lake kubwa amewalenga wanawake.

Tatu anaeleza kuwa TWCC inawahamasisha wanawake kwa kuandaa tuzo za wanawake wenye viwanda na yeye ni miongoni kati ya waliopata tuzo hiyo mwaka 2022 kwa kutengeneza bidhaa bora.



Sabrina Faraji ambaye ni Mmiliki kiwanda cha Kanga kabisa, kinachozalisha sare za mahoteli, mikoba, vyandarua na bidhaa nyingine akiwa katika moja ya majukumu yake ya ushonaji kiwandani hapo, eneo la Amani nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Anasema mwaka mwaka 2023 aliibuka kuwa mshindi wa kwanza wa bidhaa bora kwa viwanda vidogo na bidhaa iliyoshinda ni sabuni ya mwani.

"Hizi zote zimekuwa ni hamasa za kututia moyo sisi wanawake kwa kweli tunashukuru, pia naishukuru Serikali ya Zanzibar kwa sababu mwanzo kupata alama ya ubora wa bidhaa katika Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kutokana na gharama kubwa, lakini wametusiadia na sasa gharama ni nafuu," alisema.

Hivyo, aliwataka wajasiriamali wezake kuwa na utayari wa kuwa na alama ya ubora ili kupata masoko sahihi na kusaidia familia zao, lakini pia aliwataka vijana wanaomaliza masomo yao ya elimu ya juu kujifunza ujasiriamali ili kujikwamua kimaisha.

Aliongeza kwa kusema: "Mimi napokea vijana wengi wanaomaliza vyuo ambao wanakuja kujifunza na wengine hupata matumaini makubwa sana kwa sababu ajira serikalini ni chache, hivyo wasibweteke baada ya kumaliza masomo kutegemea ajira serikalini".

Aidha anasema kiwanda chake kinauwezo wa kuzalisha vipande 2,000 va sabuni kwa siku, lakini kutokana na changamoto ya mtaji huzalisha kwa mujibu wa oda anazopokea.

Mbali na hayo, anasema mwanzo wa biashara yake hiyo ilikuwa ngumu kwa sababu alipambana kupita mtaani kutangaza bidhaa zake na anasema alikutana na changamoto ya maneno ya kukatisha tamaa, lakini kwa sasa bidhaa zake zinatambulika na wateja wanamfuata yeye.

### MAFANIKIO

Anasema miongoni mwa mafanikio aliyoyapata ni kutambulika kwa bidhaa zake na kuziamini baada ya kupata alama ya ubora kutoka TBS na ZBS, kwamba amewasaidia vijana kujiajiri na kuendesha familia yake kwa kuwasomesha watoto wake.

"Mimi ni mama wa watoto watatu na sina biashara nyingine zaidi ya hii, namshukuru Mungu ya kwamba faida ninayopata nasomesha watoto wangu, lakini pia familia yangu inauwezo wa kupata milo mitatu kwa siku"alisema Tatu.

### CHANGAMOTO

Akizungumzia changamoto katika biashara hiyo, alisema ni vifungashio vya uhakika akisema visiwani Zanzibar hakuna viwanda vinavyotengeneza vifungashio, hivyo hulazimika kuagiza Tanzania Bara.

Anataja changamoto nyingine inayowaumiza wajasiriamali na masuala ya usafirishaji bandarini kodi ni kubwa wanayotozwa wanapoagiza vifungashio.

Tatu anasema soko la bidhaa zake ni Zanzibar na nje ya Zanzibar na amewahi kushiriki maonyesho mbalimbali ya Tanzania na nje ya Tanzania ikiwemo Maonyesho ya Biashara ya Afrika Mashariki.

Hata hivyo alisema soko lao pia lipo katika sekta ya utalii ambapo watalii hununua bidhaa zake kama ni zawadi, ingawa katika sekta hiyo hajawa na umaarufu katika kuzisambaza kwenye hoteli za kitalii.

Anasema malighafi anazozitumia kutengeneza bidhaa zake zipo nyingi hasa mwani ambao upo wa kutosha, lakini tatizo kubwa ni upatikanaji wa mafuta ya nazi kwa sababu bidhaa zake nyingi hutegemea mafuta ya nazi katika uzalishaji.

### USHAURI KWA WANAWAKE

Hivyo aliwataka wanawake kujiamini, kuhamasika na kusaidia familia badala ya kuwa tegemezi kwa wanaume, hivyo ni vyema wakacharika katika kujikwamua kimaisha na kiuchumi.

Sabrina Faraji (40) ni mmiliki wa kiwanda cha Kanga kabisa ambacho huzalisha bidhaa za hOtelini ikiwamo sare za wafanyakazi, mikoba, miamvuli na bidhaa zingine zinazotumika hotelini.

Anasema mwanzo alikuwa mwajiriwa katika kiwanda hicho mwaka 2006 lakini baadaye mmiliki wa awali alishindwa kukiendeleza, ndipo yeye (Sabrina) akaamua kukiendeleza tangu mwaka 2017.

"Hiki kiwanda mwanzo kilikuwa kikimilikiwa na raia wa Sweden lakini baadaye kikawashinda na wakaniachia mimi na kwa kuwa mimi ni mzawa nikaona kwa nini nisijitolee kukichukua," alisema Sabrina.

Anasema kazi ya ubunifu anaipenda, hivyo kusukuma gurudumu la maisha kuwasaidia na wenzake sita kiwandani hapo.

Sabrina anasema yeye ni mama wa watoto watatu, changamoto kubwa anayokutana nayo ni upatikanaji wa malighafi, kodi kubwa za serikali.

Anasema miongoni mwa mafanikio aliyayapata anajivunia kusomesha watoto wake, kujenga nyumba ya makazi, kuwaajiri vijana wezake kiwandani hapo na matarajio yake ya baadae ni kumiliki kiwanda kikubwa zaidi, ili kuendelea na uzalishaji wa bidhaa.

### KAULI YA SERIKALI

Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na watoto kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Siti Abass Ali anawataka wanawake nchini kujitathmini na kujitambua katika kupambana katika kujiletea maendeleo wenyewe.

Anasema katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ni lazima wanawake wajitathimini katika mwaka mzima ni kitu gani wamefanya katika kujiletea maendeleo na endapo kuna tatizo ni vyema kulitatua ili kusonga mbele kimaisha.

Siti anasema wizara huwapa mafunzo wajasiriamali wanawake, lengo ni kuwaunganisha pamoja wanawake na kupeana moyo katika maendeleo, pamoja na kupeana nguvu kwa kugombania nafasi mbalimbali za uongozi ili kuwa mbele kimaendeleo.

Anasema pia wameamua kutoa elimu hiyo kutokana na wanawake wengi kushindwa kuendesha biashara zao pamoja na kutokua na matumizi sahihi ya fedha.

Vilevile anabainisha kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafanya jitihada mbalimbali katika kuwawezesha wajasiriamali wanawake ikiwemo kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba, ili kujiendeleza katika ujasiriamali na kuachana na utegemezi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO KUPOTEA NYARAKA ZA UMILIKI VIWANJA

**SELEMANI KOLE BUNDALA** anatangaza kupotelewa na Nyaraka za Umiliki wa Viwanja, Namba **734 Kitalu "GG"** na **Namba 43 Kitalu "GG"** vilivyopo Kitangili Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaezione atoe taarifa kituo cha Polisi Kilichopo Karibu au awasiliane na Selemani kwa simu namba **078741058. Taarifa ya Polisi: PHQ/SHI/SHI/238/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya YA DODOMA**
**Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 13/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SYLIVESTER JUMA JOEL**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA TITO JOEL PHILIPO**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 mwezi 3 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 29 Mwezi 02 mwaka 2024

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 06.02.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

**Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 12 ya mwezi wa Desemba,2023**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**BARAKA LUSAJO MACHIBYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0127/0007 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAKOKO SEMINARY** mwaka ***2005.*** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/28134/2024.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI.........241......LA 2022**
**GEOFREY PAULO MIGORE....MUOMBAJI/WAOMBJI**
**DHIDI YA**

- **ISSA OMARY**
- **FATUMA SAIDI NDIKELEYE...MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

- **ISSA MUSSA OMARY**
- **FATUMA SAIDI NDIKELEYE**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**GEOFREY PAUL MIGORE** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 24/06/2024 saa 03:00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W.SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 06 Mwezi 03 ,2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**IN THE DISTRICT COURT OFDODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.....2024**
**In the matter of the Estate of the late ANGELINA JULIUS SAGENGE of Nkhungu within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOHN SOSTHENES SAGENGE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn 369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 25 TH Day of MARCH, 2024
Date at Dodoma this 28TH Day of February, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA
Kituo cha MJINI
Mkoa DODOMA
Usimamizi wa mirathi Na.18/2024
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU YAHYA SHABANI MAONWA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA
ZAITUNI HAMISI ABEDI
TANGAZO
(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 03 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 07 Mwezi 03 Mwaka 2024.

---

IN THE DISTRICT COURT OFDODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3838 /2024
In the matter of the Estate of the late EDWARD MARTIN MWANJALA of Dodoma Municipality/City at Dodoma
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SUZAN SOLOMON BISANDA

GENERAL CITATION
(Made under Rule 75 Probate Rules)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 04 Day of 04, 2024
Date at Dodoma this 07 Day of 03, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**E-MAIL: advertise@guardian.co.tz**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Afrika Kusini yaibana tena Israel

**CAPETOWN, Afrika Kusini**

AFRIKA ya Kusini imewasilisha ombi katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ), ikitaka kuchukuliwa hatua za haraka kuiamuru Israel kukubali kuruhusu misaada kuingia Ukanda wa Gaza.

Katika maombi hayo ilitahadharisha eneo hilo kukumbwa na janga la njaa na kuangamiza jamii ya Kipalestina.

Serikali ya Aftika Kusini ilisema imerudi katika Mahakama hiyo yenye makao makuu katika jiji la The Hague, nchini Uholanzi, kuomba kutolewe amri ya kuruhusiawa kwa misaada ya haraka kutokana na Wapalestina kunyimwa haki ya kupata chakula na Israel.

Taifa hilo liliishutumu Israel kuendelea kukiuka sheria za Umoja wa Mataifa za kuzuwia mauaji ya halaiki katika vita vinavyoendelea mjini Gaza.

Tangu kuanza kwa mapigano kati ya Israel na Hamas Oktoba 7, mwaka jana, Wapalestina zaidi ya 30,000 wameuwawa, wengi wao wakiwa wanawake na watoto.

Katika hatua nyingine. Waziri wa Mambo ya Kigeni wa China, Wangi Yi, ameitaka Israel kusitisha mashambulizi yake dhidi ya raia katika vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza. Yi alisema hakuna sababu ya kuendelea kwa mgogoro huo.

"Ni janga la kibinadamu na fedheha kwamba katika karne hii ya 21, madhila haya ya kibinaadamu hayawezi kukomeshwa. Hakuna sababu ya kuendelea na mgogoro huu, na hakuna kisingizio chochote cha kuendelea kuwauwa raia wasiokuwa na hatia." Alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya ukumbi wa bunge la Chila, Wang Yi alisema wafungwa wote wanapaswa kuachiwa huru na jumuiya ya kimataifa inapaswa kuunga mkono hatua za kufikia makubaliano ya kusitisha mapigano.

Aliongeza kuwa mzozo unaoendelea kati ya Israel na Hamas unaweza kusuluhishwa kupitia utekelezwaji kikamilifu wa mkataba wa kimataifa wa kuunda mataifa mawili.

Waziri huyo alisema azma ya Wapalestina ya kuwa dola huru haiwezi kuepukika.

Hata hivyo, mapigano makali yanaendelea kushuhudiwa katika maeneo ya Ukanda wa gaza, wakati juhudi za kusitisha mapigano zinaendelea.

Jeshi la Israel, ambalo limeapa kuliangamiza kundi la Hamas liliendelea na kushambulia Ukanda wa Gaza kwa mabomu na makombora usiku kucha na kusababisha hali kuwa mbaya Zaidi.

Wakazi wa mji wa Khana Younis eneo ambalo nyumba zake zilijengwa kwa ufadhili wa Qatar, waliripoti kusikia miripuko ya mabomu na makombora usiku mzima wa kuamkia Alhamisi.

Ndege za kijeshi za Israel zilishambulia pia maeneo ya kambi ya wakimbizi ya Al-Nuseirat na mji wa Deir Al-Balah katikati ya Ukanda wa Gaza, na sehemu za mji wa kusini wa Rafah.

Wakati mashambulizi hayo yakitikisa miji hiyo, mazungumzo ya kusitishwa mapigano yaliendelea katika mji wa Cairo nchini Misri.

Wawakilishi wa Hamas na wajumbe kutoka Qanchi za Qatar na Marekani walikutana kujadili suala hulo, huku Israel ikiususia.



Misaada michache ikifikishwa katika eneo la Ukanda wa Gaza kwa kutumia njia ya anga hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

# Senegal kumchagua rais Machi 24

**DAKAR, Senegal**

SERIKALI ya Senegal imetangaza kuwa uchaguzi wa rais katika nchi hiyo utafanyika Machi 24, mwaka huu.

Tangazo hilo limetolewa baada ya kuwepo kwa hali ya mvutano nchini humo baada ya Rais Macky Sall, kuahirisha uchaguzi uliotakiwa kufanyika mwezi uliopita, na kusababisha maandamano nchi nzima.

Rais Sall, ambaye muhula wake unamalizika Aprili 2, alisisitiza kuahirisha uchaguzi huo hakunuia kugombea muhula wa tatu.

Wapinzani wake walimshutumu kwa kile walichokiita kuandaa mapinduzi ya kikatiba.

Senegal imeonekana kwa muda mrefu kama mojawapo ya nchi zenye demokrasia imara zaidi barani Afrika.

Ni nchi pekee katika Afrika Magharibi ambayo haijawahi kuwa na mapinduzi ya kijeshi.

"Rais wa Jamhuri aliarifu Baraza la Mawaziri kwamba tarehe ya uchaguzi wa urais ilikuwa imepangwa Jumapili Machi 24," ilisemataarifa ya baraza la mawaziri. he 2 Aprili.

Jumatano jioni Rais Sall alivunja serikali na kumteua Waziri Mkuu mpya, Amadou Ba na Waziri wa Mambo ya Ndani Sidiki Kaba.

Rais Sall amehudumu kwa mihula miwili kama kiongozi wa Senegal baada ya kuchaguliwa kwa mara ya kwanza mwaka 2012, akiahidi kuwa hatakaa madarakani kwa kwa muda mrefu.

***BBC***

**"Rais wa Jamhuri aliarifu Baraza la Mawaziri kwamba tarehe ya uchaguzi wa urais ilikuwa imepangwa Jumapili Machi 24," ilisemataarifa ya baraza la mawaziri. he 2 Aprili.**

# Niger, Mali, Burkina Faso kuunda jeshi la pamoja

**NIAMEY, Niger**

NCHI za Niger, Mali na Burkina Faso zimeamua kuunda kikosi cha pamoja cha kijeshi kwa ajili ya kupambana na wanamgambo wa kijihadi.

Mkuu wa jeshi la Niger, Moussa Salaou Barmou, alitangaza kuwa kikosi hicho kitaanza kazi haraka iwezekanavyo, lakini hakutoa maelezo zaidi.

Makundi yenye uhusiano na Islamic State na al-Qaeda yamefanya mashambulizi ambayo yameua maelfu ya watu katika eneo hilo mwaka uliopita.

Serikali za kijeshi katika nchi hizo tatu, zimezidi kuimarisha ushirika wao wa karibu katika miezi ya hivi karibuni.

Mwaka uliopita, nchi hizo zilitiliana saini mkataba wa ulinzi wa pamoja unaojulikana kama Muungano wa Mataifa ya Sahel, na kujiondoa kutoka katika kikosi cha kimataifa kinachofahamika kama G5.

Ghasia katika eneo hilo la Afrika Magharibi limezidi kuwa mbaya katika miaka ya hivi karibuni licha ya ahadi za kukabiliana na mzozo huo uliodumu kwa muongo mmoja.

Nchi hizo zimesitisha uhusiano wao na Ufaransa, ambayo ilizitawala zamani na ilisaidia kupambana na makundi hayo kwa kutumia majeshi yake.

Ujumbe wa Umoja wa Mataifa wa kulinda amani nchini Mali, Minusma, ambao ulikuwa umekuwepo kwa zaidi ya muongo mmoja pia uliamriwa na viongozi wa nchi hiyo kujiondoka haraka.

Hata hivyo, nchi hizo zimekuwa na uhusiano imara nan chi ya Russia ambayo kwa kutumia kundi la Wagner limeziba pengo la vikosi vua kijeshi vya Ufaransa.

***BBC***

# KOCHA PRISONS AFICHUA ALIPOIKAMATA SIMBA

**Na Faustine Feliciane, MOROGORO**

BAADA ya kushuhudia timu yake iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 mbele ya Simba juzi, Kocha wa Tanzania Prisons, Hamad Ally amefichua mbinu aliyoitumia kuwabana wapinzani wake na kufanikiwa kupata ushindi huo.

Kocha huyo alisema udhaifu wa mabeki wa Simba kuchelewa kurudi kukaba wanapoenda kushambulia ndio ukiompa matokeo mazuri juzi.

Ally alisema kwa muda aliisoma Simba na kujua ubora wao na ndio dhaifu wao na kutoa maelekezo kwa wachezaji wake kwenye uwanja wa mazoezi kuelekea kwenye mchezo huo uliochezwa uwanja wa Jamhuri.

"Tulifanyia kazi mazoezi udhaifu wa Simba, tulikuwa mabeki wa Simba hasa wa pembeni ni wazuri kwenye kushambulia, lakini huwa wanachelewa kurudi kukaba. Sisi tuliwaandaa mawinga wetu na washambuliaji wawe shapu kukimbia na mpira kuelekea lango la Simba, na tumefanikiwa, tumeshinda kwa mashambulizi ya kushtukiza, nawapongeza wachezaji wangu kwa kufuata maelekezo na kazi nzuri waliyoifanya," alisema Ally.

Alisema Simba wanapaswa kufanya marekebisho mapungufu hayo ili kuweza kuendelea kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa wanayoshiriki.

"Simba ni timu nzuri, huwezi kubeza ubora wao, lakini lazima mapungufu madogo madogo kama haya wayafanyie kazi, ni moja ya wawakilishi wa Tanzania kwenye mashindano ya CAF, lazima wafanye kazi haya," alisema Ally.

Aidha, kocha huyo amesema kwa sasa wanaelekeza nguvu zao kwenye mchezo wao inayofuata dhidi ya Mtibwa Sugar watakaocheza nao kwenye uwanja wa Manungu Mkoani hapa.

"Ushindi wa mechi hii ni chachu kwetu kuelekea kwenye mchezo unaofuata, hatupaswi kubweteka kwa sababu tumemfunga Simba, tunaenda kujiandaa kwa mchezo unaofuata," alisema Kocha huyo.

Matokeo ya juzi yameifanya Prisons kufikisha pointi 27 na katika nafasi ya sita ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.



Baadhi ya vijana wa makundi ya jogging wakifanya na mazoezi ya viungo kwenye viwanja vya Leader's Club jijini Dar es Salaam bàada ya kumaliza kukimbia mbio za kilomita tano juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Singida yatimua benchi lote la ufundi

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya matokeo mabovu ya timu yao, klabu ya Singida Fountain Gate imeamua kutimua benchi lote la ufundi akiwemo Kocha Mkuu, Thabo Senong.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, ikisainiwa na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano, Hussein Massanza, imesema kuwa imeamua kufanya hivyo kwa maslahi ya klabu hiyo. Hata hivyo, taarifa hiyo haijasema kwa sasa timu hiyo itashikiliwa na nani katika kipindi hiki cha mpito.

Taarifa ya klabu hiyo imetoka siku chache baada kupata kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, mechi iliyochezwa Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, ambao timu hiyo inautumia kwa sasa kama wa nyumbani.

"Bodi na Menejimenti ya Klabu ya Singida Fountain Gate, imefikia uamuzi wa kuvunja benchi lote la ufundi lililokuwa kiliongozwa na Thabo Senong kufuatia mfululizo wa matokeo mabaya.

Kufuatia uamuzi huu, uongozi utatangaza benchi jipya la ufundi muda wowote kutoka sasa," ilisema taarifa hiyo.

Mara ya mwisho kushinda ilikuwa ni Novemba 27 mwaka jana, ilipoifunga Coastal Union mabao 2-1 nyumbani, na hadi leo hii haijaonja ladha ya ushindi ikicheza mechi nane, ikipoteza tano na sare tatu.

Disemba Mosi mwaka jana, ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya JKT Tanzania, na sare nyingine na mechi inayofuata ikatoka suluhu dhidi ya KMC, kabla ya kwenda kukutana na kipigo cha bao 1-0, Uwanja wa Nyankumbu, Geita, dhidi ya Geita Gold.

Ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, kabla ya kupata kipigo kingine cha mabao 3-1 dhidi ya Prisons, na kwenda kutoa sare ya bao 1-1, dhidi ya Taboara United.

Baada ya hapo ikachapwa bao 1-0 dhidi ya Azam kabla ya kubamizwa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar.

## Riadha kupaa kuelekea Ghana

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya mchezo wa riadha inatarajiwa kuanza safari mwishoni mwa wiki hii kuelekea Accra nchini Ghana kushiriki mashindano ya michezo ya Afrika (All African Games) yatakayoanza leo.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu wa Rais wa Shirikisho la mchezo wa riadha Tanzania, William Kalage alisema timu yao imeweka kambi ya muda mrefu mkoani Arusha ili kwenda kuipeperusha vema bendera ya Taifa.

"Timu yetu imefanya maandalizi ya muda mrefu kuhakikisha inapata nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano huyo, alisema Kalage.

Rais huyo alisema endapo timu hiyo itafanya vema italiheshimisha Taifa la Tanzania kupitia mchezo huo na kuwataka wanariadha hao kufuata vizuri maelekezo waliyopewa na walimu wao.

Katika hatua nyingine alisema kuwa Kamati mbili zilizoundwa na Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa migogoro inayoendelea ndani ya vyama vya michezo.

## Ligi Kuu Z'bar kusimama kupisha mfungo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI KUU ya Zanzibar itakwenda mapumziko takribani mwezi mmoja na nusu kwa kwasababu ya kupisha mfungo wa mwezi wa Ramadhani ambao unatarajiwa kuanza kati ya Machi 11 au 12.

Ni utamaduni wa hapa Zanzibar katika mwezi huo Ligi zote rasmi husimama ili kuwapa nafasi watu wote kutekeleza ibada hiyo ya funga ambayo ni nguzo ya nne katika Uislamu.

Ligi hiyo inasimama ikiwa timu zote 16 zimecheza michezo 20 na zimebakisha michezo 10 ambayo itaendelea baada ya kumaliza mwezi wa Ramadhani.

Wakati Ligi hiyo inasimama bado mbio za ubingwa zimeendelea kushika kasi kwa timu nne za juu katika msimamo wa Ligi na joto la kushuka daraja likiendelea kupanda kwa timu nne ambazo zipo chini katika msimamo huo.

Maafande wa JKU ambao ndio vinara wa Ligi hiyo wameendelea kupunguzwa kasi kwa baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Maafande wa Mafunzo mchezo uliochezwa katika uwanja wa Mau B.

Wakati huo huo Maafande wa Zimamoto nao wameshindwa kutamba dhidi ya KVZ FC kwa kulazimisha sare ya bao 1-1 mchezo uliochezwa katika uwanja wa Mau A.

## ZISIKUPITE

### ARTETA ATAKIWA BARCA

BARCELONA a bado wanavutiwa na kocha wa Arsenal, Mikel Arteta kuchukua nafasi ya Xavi, ambaye anaondoka mwishoni mwa msimu huu, lakini klabu hiyo ya Hispania inajua itakuwa vigumu kumteua. ***(Relevo)***

### SOUTHGATE ATAJWA MAN

KOCHA wa England, Gareth Southgate na wa Brentford, Thomas Frank ni miongoni mwa chaguzi zinazozingatiwa na Manchester United ikiwa wataamua kuachana na Erik ten Hag mwishoni mwa msimu huu. ***(ESPN)***

### KIMMICH AWINDWA

LIVERPOOL, Arsenal na Manchester City zinapigana vikumbo kumsajili kiungo wa Bayern Munich, Joshua Kimmich. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 29 anatazamia kuondoka Bavaria msimu huu wa joto. ***(Express)***

### ZERBI BEI KUBWA

KLABU yoyote inayotaka kumwajiri kocha mkuu wa Brighton, Roberto de Zerbi msimu huu wa joto italazimika kuwalipa Seagulls hao pauni milioni 12.8. Barcelona, Liverpool na Manchester United zimehusishwa na Muitaliano huyo. ***(Mirror)***

### ALONSO HUYO BAYERN

KLABU ya Bayern Munich iko mbele ya Liverpool katika kinyang'anyiro cha kumteua Xabi Alonso kama kocha wao ikiwa Muhispania huyo ataamua kuondoka Bayer Leverkusen msimu wa joto. ***(Telegraph)***

### HUGHES KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL ina nia ya kumteua Richard Hughes kama mkurugenzi wa michezo baada ya yeye mwenyewe 44, kuthibitisha kuwa ataacha nafasi yake kama mkurugenzi wa kiufundi wa Bournemouth mwishoni mwa msimu huu. ***(Times)***

### VARELA AGOMBEWA

L8IVERPOOL, Borussia Dortmund na Paris St-Germain zinamtaka kiungo wa kati wa Argentina, Alan Varela mwenye umri wa miaka 22, lakini watalazimika kuilipa Porto kifungu chake cha pauni milioni 60. ***(Mercato)***

### JOELINTON KUBAKI

KIUNGO wa kati wa Brazil, Joelinton anataka kubakia katika Ligi Kuu ya England ikiwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 hatakubali mkataba mpya zaidi ya 2025 na Newcastle United. ***(Football Insider)***

### WILLIAMS AWANIWA

CHELSEA inataka kumsajili winga wa Athletic Bilbao, Nico Williams. Mshambuliaji huyo wa Uhispania mwenye umri wa miaka 21 ana kipengele cha kutolewa ambacho kinaweza kumaanisha kuwa anapatikana kwa pauni milioni 43 msimu huu wa joto. ***(Telegraph)***

### REUS HUYO WEST HAM

WEST Ham imepewa nafasi ya kumsajili winga wa Borussia Dortmund Mjerumani Marco Reus mwenye umri wa miaka 34 mara mkataba wake utakapokamilika msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

### HENDERSON HAJUTII

KIUNGO wa kati wa Ajax, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 33, hajutii kuondoka Liverpool, akisema ulikuwa „uamuzi bora" kwa pande zote. ***(Guardian)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE: SINA TATIZO NA KOCHA ENRIQUE

Asema ana matatizo mengi, lakini kocha huyo wala hahusiki...

KYLIAN Mbappe amesisitiza kuwa uhusiano wake na Luis Enrique ni ‚mzuri' licha ya ripoti za hivi karibuni za machafuko katika vyumba vya kubadilishia nguo.

Mbappe hivi majuzi alithibitishia PSG kwamba ana nia ya kuondoka katika klabu hiyo baada ya kumalizika kwa mkataba wake Juni.

Mshambuliaji huyo nyota tangu wakati huo amekuwa akihusishwa na kuhamia Real Madrid, huku ripoti zikisema kwamba tayari amekubali mkataba wa miaka mitano na Los Blancos wenye thamani ya euro milioni 15 kwa mwaka.

Kufuatia uthibitisho kwamba Mbappe anakaribia kuondoka PSG, kocha Enrique inaonekana mara moja alianza kupanga maisha bila fowadi wake nyota.

Akiwa Mbappe hajaanza katika ushindi wa 2-0 dhidi ya Nantes, Enrique kisha akachagua kumtoa katika sare ya bila kufungana na Rennes na Monaco.

Akizungumza na Canal Plus siku ya Jumanne, Enrique alithibitisha nia yake ya kujiandaa kutokuwa na Mbappe kwenye vitabu vya Parc des Princes msimu ujao, akisema: „Kylian atafunga mabao 50, kutoa pasi 25 za mabao na kocha yeyote, timu yoyote. Inaonekana mustakabali wake wa hivi karibuni. haitakuwa hapa kwa hivyo itabidi tujaribu suluhisho zingine."

Uvumi umeenea kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa mfarakano katika uhusiano wa Mbappe na Enrique kutokana na hilo.

Baada ya ushindi wa PSG wa hatua ya 16 bora wa Ligi ya mabingwa Ulaya dhidi ya Real Sociedad Jumanne jioni, Mbappe alikanusha uvumi wa kushindwa katika mahojiano na Canal Plus.

"Uhusiano wangu na kocha ni mzuri," alisisitiza Mbappe. „Hakuna tatizo hata kama watu wanaweza kudhani kuwa lipo. Nina masuala mengi lakini kocha si mmoja wao."

Hili la Mbappe limekuja baada ya wawili hao kuripotiwa kufanya mazungumzo ya wazi baada ya fowadi huyo kumweleza kocha wake kuhusu kutoridhishwa na nafasi yake ya sasa katika klabu hiyo.

# JORGINHO ALIFURAHISHWA KUHUSISHWA BARCELONA

**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Jorginho atakuwa tayari kujiunga na Barcelona msimu huu wa joto, kwa mujibu wa ripoti kutoka Hispania.

Mkataba wa Jorginho unamalizika mwishoni mwa msimu huu, ingawa washikabunduki walibakiza chaguo la kuongeza mkataba huo kwa mwaka mmoja na inasemekana kuwa mazungumzo yanaendelea kuhusu mkataba mpya kufuatia kampeni nzuri ya 2023/24.

Iwapo kiungo huyo hatakubali masharti mapya, huenda akawa analengwa na Barcelona.

Kwa mujibu wa ripoti La Blaugrana inajitayarisha kwa dirisha lingine la majira ya joto huku kukiwa na kupungua kwa matumizi na usajili utakuwa wa ‚dhahiri', jambo ambalo linafanya dili la bure au la chini kwa Jorginho kuvutia zaidi.

Barcelona walimtazama Jorginho kama mbadala wa Gavi aliyejeruhiwa wakati wa dirisha la Januari lakini hatimaye wakaamua kutokubali dili hilo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia ‚atafurahi' kujiunga na Barca akiwa alikaribia kusajiliwa mwaka 2018 kabla ya kuhamia Chelsea, ripoti hiyo inaongeza.

Usajili wowote wa Jorginho unakwenda kinyume na malengo ya mkurugenzi wa michezo Deco ya kutoleta mchezaji yeyote mwenye umri wa zaidi ya miaka 30, lakini hili linaonekana kuwa suala la kipekee kwani hitaji la kiungo mpya ni kubwa.

Huku dirisha lingine lililowekewa vikwazo likikaribia, Barcelona wamesitisha mpango wa kumnunua Amadou Onana wa Everton.

Klabu hiyo bado ina matumaini ya kuleta winga anayetumia mguu wa kushoto na kumsajili Joao Cancelo kwa mkataba wa kudumu kufuatia mkopo wake kutoka Manchester City.

Barcelona hawatarajii kufanya uhamisho wa fedha nyingi isipokuwa wachezaji muhimu kama vile Frenkie de Jong na Ronald Araujo.

Ingawa kazi ya kupanga kikosi inaendelea, Barcelona pia wanatafuta kocha mkuu kuchukua nafasi ya Xavi mwishoni mwa msimu.



## Bellingham afungiwa mechi mbili

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Jude Bellingham amefungiwa michezo miwili ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya kuoneshwa kadi nyekundu kwenye sare ya 2-2 dhidi ya Valencia wiki iliyopita.

Bellingham mwenye umri wa miaka 20, alidhani alikuwa amefunga bao la ushindi dakika sita baada ya dakika za lala salama pale Mestalla Jumamosi.

Lakini mwamuzi Gil Manzano alikuwa amepuliza kipenga cha kumaliza mchezo wakati mpira ukiwa hewani.

Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF) lilisema Bellingham alioyesha „dharau au kutomjali" Manzano wakati wachezaji na makocha wa Real walipomzunguka.

Bellingham, ambaye alikuwa akirejea baada ya wiki tatu nje ya uwanja kutokana na jeraha la kifundo cha mguu, alipigwa faini ya euro 600 na Real euro 700.

Real ilikata rufaa dhidi ya kadi nyekundu ya Bellingham, lakini kamati ya nidhamu ya RFEF ilitupilia mbali hoja yao.

Kocha Carlo Ancelotti alisema baada ya tukio hilo: „Tulichukizwa na kadi nyekundu ya Bellingham kwa sababu hakusema neo lolote la matusi. Ilikuwa ni kufadhaika."

Mfungaji bora wa Real msimu huu akiwa na mabao 16 kwenye ligi, Bellingham atakosa mechi dhidi ya Celta Vigo Jumapili na Osasuna Machi 16.

Atapatikana kwenye mchezo dhidi ya Athletic Bilbao Machi 31 kufuatia mapumziko ya kimataifa.




## Bayern Munich kuizidi kete Liverpool

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA Xabi Alonso ameripotiwa kuanzisha mazungumzo na Bayern Munich na kuibua hofu huenda akapiga chini mpango wa Liverpool wa kumtaka akarithi mikoba ya Jurgen Klopp.

Raia huyo wa Hispania yupo kwenye rada za klabu hizo mbili, Bayern Munich na Liverpool wakitaka huduma yake baada ya kufanya kweli akiwa na kikosi cha Bayer Leverkusen huko kwenye Bundesliga.

Kikosi hicho cha Alonso kwa sasa kinaongoza msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwa tofauti ya pointi 10 dhidi ya timu inayoshika nafasi ya pili, Bayern na haijapoteza mechi yoyote msimu huu 2023/24.

Hata hivyo, Bayern wamepanga kuwadhoofisha wapinzani wao hao, Leverkusen kwa kuanzisha mazungumzo ya kumchukua Alonso akawe kocha wao kuanzia msimu ujao.




Bayern imethibitisha itaachana na Thomas Tuchel mwishoni mwa msimu huu. Sasa mjadala ni namna Alonso atakavyokwenda kuwa kocha wao mpya.

Kiungo huyo wa zamani wa Liverpool alishinda mataji matatu wakati anaichezea Bayer kati ya mwaka 2014 na 2017.

Liverpool nao wanaamini kwa kuwa aliwahi kucheza kwenye timu yao pia, basi wanaweza kumshawishi akatua Anfield kuchukua mikoba ya Klopp, atakayeachana na miamba hiyo mwishoni mwa msimu.

Alonso anafahamnu pengo atakaloacha Klopp kwenye kikosi cha Liverpool ni kubwa sana kuliziba.

Mkataba wa Alonso huko BayArena utafika tamati 2026 na kama kuna timu inamhitaji basi itapaswa kulipa fidia kati ya Pauni 13 milioni na Pauni 21 milioni.

# AZAM YAIBIPU YANGA, FEI TOTO HASHIKIKI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

SARE ya bao 1-1 iliyoipata juzi usiku Azam FC kwenye uwanja wake wa nyumbani, Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam dhidi ya Coastal Union imeifanya timu hiyo kukaa juu ya msimamo wa Ligi Kuu, huku ikisubiriwa mechi ya leo kati ya Namungo FC dhidi ya Yanga.

Dakika tisa kabla ya mechi kumalizika, Feisal Salum aliisawazishia Azam bao, akiiokoa timu yake kwa kipigo, lakini akifikisha idadi ya mabao 12 na kuzidi kumuacha Stephane Aziz Ki wa Yanga aliyeongoza kwa kipindi kirefu, akiwa na mabao 10.

Kabla ya bao hilo, Coastal Union ilipata bao dakika ya 68 lililowekwa wavuni na Semfuko Charles.

Matokeo hayo yameifanya Azam kuongoza ligi, ikifikisha pointi 44, ikiiacha Yanga ikiwa na pointi 43, kabla ya kucheza mechi ya leo ugenini, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Lindi ambapo, matokeo ya mchezo huo yataamua kama Wanalambalamba wataendelea kusalia kileleni au la.

Fei Toto amefikisha mabao 12, akiwa pia ametoa pasi za mwisho tano kwa timu yake, hivyo kuchangia jumla ya mabao 17 kwenye timu yake ya Azam aliyojiunga nayo msimu huu akitokea Yanga.

„Nafurahi kufunga mabao na kuisaidia timu yangu, na hata kama itatokea nikawa mfungaji bora ni vizuri pia, mimi ni mpambanaji, kawaida yangu kupambana wala sishindani na mtu, ninachofanya ni kuipeleka juu Azam, ikitokea nikichukua kiatu cha dhahabu sawa, akichua mwingine wala sitokuwa na kinyongo," alisema Fei Toto.

Aziz Ki wa Yanga ametupwa nafasi ya pili kwa mabao 10, Jean Baleke aliyekuwa akiichezea Simba, Maxi Nzengeli wa Yanga, Waziri Junior wa KMC na Marouf Tchakei wa Tabora United ambao wote wana mabao manane.

Wachezaji wenye mabao saba ni Prince Dube wa Azam FC, Adam Adam wa Mashujaa na Samson Mbangula wa Prisons.

Baada ya sare ya bao 1-1 jana dhidi ya Azam, Coastal Union imekwea hadi nafasi ya nne ya msimamo ikiwa na pointi 27 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.




Benchikha

## Kocha Simba alia uzembe

INATOKA UK. 24

kwenye michezo hiyo.

Baada ya mechi ya juzi Simba sasa itasafiri kwenda Tanga kukabiliana na Coastal Union kwenye uwanja wa Mkwakani kesho Jumamosi.

Halafu watarejea tena Morogoro kucheza na Mashujaa ikiwa mfululizo wa michezo minne ya Ligi Kuu Tanzania Bara kabla ya kugeukia mashindano ya Ligi ya mabingwa Afrika.

Shirikisho la Soka Afrika, CAF, linatarajiwa kuchezesha droo ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika machi 12 ambapo Simba huenda ikakutana na timu mojawapo kati ya Mamelod Sundowns, Petrol Atletico de Luanda au Al Ahly.

Michezo ya mkondo wa kwanza wa michuano hiyo inatarajiwa kucheza kati ya Machi 29 na 30 mwaka huu mbapo Simba itaanzia nyumbani.

## Ligi ya Mabingwa Mikoa kuanza kutimua vumbi leo

**Na Mwandishi Wetu**

LIGI ya Mabingwa Mikoa hatua ya makundi inatarajia kuanza kutimua vumbi katika vituo vinne nchini ambavyo ni Njombe, Pwani, Manyara na Mwanza, huku Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1986, Tukuyu Stars ikitarajiwa kucheza dhidi ya Don Bosco, Uwanja wa Sabasaba, Njombe.

Jumla ya timu 16 zinatarajiwa kushuka uwanjani leo katika mechi nane zitakazochezwa kwenye vituo vyote katika kusaka timu zitakazopanda kwenda Ligi Daraja la Pili, maarufu kama ‚first league', msimu ujao. Wakati Tukuyu Stars ikiwa Kundi A, ikitarajiwa kucheza dhidi ya Don Bosco, katika kundi hilo hilo, timu ya Hausing itakipiga dhidi ya Tutes Hub kwenye uwanja huo huo wa Sabasaba baada ya mechi ya kwanza.

Timu ya Black Six, itaifungua ligi hiyo kwenye Uwanja wa Tamco, Kibaha mkoani Pwani, itakapocheza dhidi ya Kiduli FC, na baadaye Gunnes FC wataingia kucheza dhidi ya Red Angles, mechi zikiwa ni za Kundi B.

Kundi C, ambalo lipo Babati mkoani Manyara litafungua mechi zake za ligi leo, wakati Reggae Boys itakapokwaana na Arusha City, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa na baadaye kutapigwa mechi katika Kawele FC dhidi ya Veteran Middle Age kwenye uwanja huo huo.

Mechi za Kundi D zitapigwa leo uwanja wa Nyamagana, Mwanza, wakatiRock Solution itakapocheza dhidi ya Bweri FC na Kandahari itakipiga dhidi ya Mbarali Ushirikiano.




Wachezaji wa Real Madrid, Nacho (kushoto) na Jude Bellingham wakishangilia baada ya timu yao kupata sare ya 1-1 na RB Leipzig na kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga hesabu zao ni ponti tatu leo

INATOKA UK. 24

mzuri na kuwapa ushindani mkubwa na kufanikiwa kupata bao dakika za mwisho.

"Tumefanya maandalizi mazuri kukabiliana na Namungo, tunawafahamu mechi ya kwanza walitusumbua na sasa tunaingia kivingine kuhakikisha tunavuna pointi tatu ugenini," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Namungo, Mwinyi Zahera alisema wachezaji wake wapo tayari kwa mchezo huo kuhakikisha wanatumia vema uwanja wa nyumbani.

"Tumefanya maandalizi mazuri, tunatambua ubora wa Yanga lakini pia wanamadhaifu tutayatumia na kupambana kupata matokeo mazuri mbele ya Yanga," alisema Zahera.

Michezo
Ijumaa Machi 8, 2024
Nipashe

## Mbappe: Sina tatizo na Enrique

UKURASA 21





Wachezaji wa Yanga, Farid Musa (kushoto) na Zawadi Mauya wakiwa uwanja wa ndege wa Julius Nyerere jana wakielekea mkoani Lindi kwenye mchezo wao dhidi ya Namungo FC utakaopigwa leo. **PICHA: YANGA**

# KOCHA SIMBA ALIA UZEMBE

## ●●●Asema safu ya ulinzi ilifanya makosa, walimiliki mpira lakini...

**Na Faustine Feliciane, MOROGORO**

KOCHA msaidizi klabu ya Simba, Selemani Matola, amesema uzembe mdogo wa safu yao ya ulinzi umewagharimu kwenye mchezo wao wa juzi dhidi ya Tanzania Prisons na kujikuta wakipokea kipigo cha mabao 2-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Matokeo hayo yaimefanya Simba kufikisha pointi 36 baada ya kushuka dimbani mara 16 ikishika nafasi ya tatu mbele ya Azam FC wanaoongoza msimamo na Yanga iliyopo nafasi ya pili.

Matola alisema licha ya kucheza vizuri na kumiliki mpira, bado walikuwa na makosa kwenye kujilinda hasa wakiwa wanakwenda kushambulia kwa mpinzani wao.

„Ni matokeo ya mpira, tumecheza vizuri lakini makosa ya mabeki wetu yametugharimu, tunaenda kufanyia kazi makosa yetu na kurejea kwenye ubora wetu, tulitengeneza nafasi nyingi tumeshindwa kuzitumia na wenzetu wamepata nafasi chache wamezitumia, tunawapongeza,“ alisema Matola.

Matola alisema kupoteza mchezo huo sio mwisho wa mapambano na kwamba bado wanamichezo mbele yao hivyo lazima warejee haraka kwenye hali yao ili kuweza kupata ushindi

INAENDELEA UK. 23

# Yanga hesabu zao ni ponti tatu leo

**Na Saada Akida**

YANGA leo wataingia kivingine katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC wakiwa na kumbukumbu ya kupata pointi dakika za mwisho kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza dhidi ya wapinzani hao.

Katika mchezo wa mzunguko wa kwanza wa ligi kuu Yanga ikiwa uwanja wa nyumbani walikutana na kibarua kigumu na kuvuna alama tatu kwa ushindi wa bao 1-0 dakika za mwisho katika dimba la Azam Complex Chamazi Dar es Salaam.

Kikosi cha Yanga kimeondoka jana kwa ndege kuelekea Nachingwea na hapo watapanda basi moja kwa moja kwenda Ruangwa tayari kwa mchezo huo leo kwenye uwanja wa Majaliwa.

Yanga wanahitaji ushindi katika mchezo huo kwa lengo la kuwaacha mbali kwenye mbio za ubingwa wapinzani wao Azam FC wenye pointi 43 sawa na mabingwa hao watetezi wakiwa mbele kwa michezo mitatu.

Timu hizo zimekutana mAziz-Kio tangu mwaka 2021 hadi 2023 na wametoka sare mechi moja ikiwa Novemba 20, 2021 ambapo walifungana 1-1.

Aprili 22 na Desemba 17, 2022 Yanga walishinda mechi zote mbili nyumbani na ugenini, walivuna alama tatu kwa ushindi wa mabao 2-1 na mzunguko wa pili Namungo FC wakiwa nyumbani waliruhusu mabao 2-0.

Februari 4, mwaka jana Yanga walifanikiwa kuvuna pointi zingine wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 na Septemba 20 katika mchezo wa mzunguko wa kwanza msimu huu walipata alama zote tatu.

Kuelekea mchezo wa leo Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi alisema maandalizi yameenda vizuri malengo makubwa na kuendelea na safari yao ya kukusanya pointi kila mechi kwa ajili ya kutetea ubingwa.

Alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu mechi ya duru la kwanza Namungo FC walionesha mchezo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >